# Mwongozo kwa Waalimu

## Wakati na Biblia Daraja 0, la kwanza na la pili

Mfululizo wa B

Masomo ya saba hadi kumi na mbili

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)
Imesajiliwa kama shirika la Hisani Uingereza (Namba 1186004)

**Dhamira**
Kuandaa masomo ya Biblia kwa ajili ya wadau ili kutumika kuwakilisha kweli ya Yesu Kristo kwa kizazi kijacho ulimwenguni kote.

**Maono**
Kufikia kizazi kijacho kwa lugha zao kwa kutumia mtaala wetu kamili kwa kukuza na kusaidia mtandao wa kimataifa wa wabia wanaojitolea.

## HABARI KWA UJUMLA

**Bible Educational Services hufanya nini:**

Bible Educational Services (BES) huchapisha masomo ya Biblia ya "Wakati na Biblia/Bibletime", "Maisha Mapya/New Life" na "Wakusanyaji/Gleaners" kwa Lugha ya Kiingereza na kusaidia vituo vya Shule ya Biblia kwa njia ya Posta pamoja na mashirika mengine ya namna hiyo yanayotumia masomo ya BES huko Uingereza na nchi zingine. BES hufanya hivi kwa kutembelea, kutoa ushauri, kutoa mafunzo na kuunganisha mashirika haya na mengine. Sasa hivi, BES inafanya kazi na vikundi mbalimbali kutoka nchi zingine, vinavyohusika na kutafsiri, kubuni, kuchapisha na kusambaza masomo. Masomo haya yanatolewa bure kabisa kwa kila mtoto.

Kwa mara ya kwanza, masomo ya Wakati na Biblia yalitumika huko Kusini mwa Ireland (Uingereza) zaidi ya miaka sitini iliyopita. Bible Educational Services (BES) wameendelea kuchukua jukumu la uhariri wa masomo ya Wakati na Biblia kwa lugha ya Kiingereza na Lugha zingine. Kwa muda mrefu, Masomo ya Wakati na Biblia (Bibletime) yalichapishwa kwenye muundo wa A4 ambao uliwawezesha wanafunzi kutoka baadhi ya maeneo kutuma masomo yao kwenye kituo cha BES kwa ajili ya kusahihishwa kila baada ya wiki nne. Hivi karibuni, masomo ya miezi sita yamechapishwa kwa muundo wa A5. Muundo huu umefanya utumiaji wa masomo haya uwe rahisi na wa kufaa zaidi kwa makanisa na shule ambazo hazina ufanisi mzuri wa mfumo wa njia ya posta. Tunawashukuru Every Home Crusade au Revival Movement huko Belfast Uingereza kwa kutuwezesha kufanya hivi.

Masomo ya BES ni ya kipekee kwa sababu yameandaliwa ili kutumika nyumbani au kwenye vikundi kama vile kutoka kwenye makanisani na kwenye shule. Masomo haya yameandaliwa kwa kuzingatia vyema mtaala (Syllabus). Masomo yamepangiliwa vizuri na unaomruhusu mwanafunzi kuyatumia hadi atakapotimiza umri wa miaka 20. Masomo yanapatikana katika madaraja matano ambayo yamezingatia umri tofauti. Nayo ni, masomo kwa ajili ya watoto wa chekechea (Daraja 0) ambao wana umri wa chini ya miaka mitano, miaka mitano hadi saba (Daraja la 1), miaka nane hadi kumi (Daraja la Pili), miaka kumi na moja hadi kumi na mitatu (Daraja la Tatu) na miaka kumi na minne hadi kumi na sita (Daraja la Nne). Kuna Mtaala wa miaka mitatu katika kila kikundi cha umri (angalia ukurasa wa 4). Vikundi hivi vya umri vinaweza kutofautiana kulingana na uwezo tofauti wa watoto. Rasilimali na masomo ya Wakati na Biblia yanawapa watoto fursa ya kujifunza Neno la Mungu, kujifunza Habari za Biblia na kujifunza kukabiliana na changamoto zinazotokea maishani mwao kulingana na mwongozo wa Injili ya Bwana Yesu Kristo.

Nakala zilizochapishwa za masomo kwa Lugha ya Kiingereza zinapatikana kwenye tovuti ya BES /BES website – www.besweb.com au kwa katibu ofisi ya BES Uingereza. Yanapatikana pia kwa lugha zingine kwenye tovuti. Kwenye tovuti kuna nyaraka muhimu kwaajili ya mtu yeyote au shirika linalopenda kushirikiana nasi.

## Anuani za mawasiliano za BES


**Ofisi ya Uingereza (Northern Ireland) (Mhifadhi wa masomo yote ya Kiingereza)**
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Simu: +44 286 632 2462

**Katibu wa Uingereza**
Bw. Stephen Gillham,
Barua pepe: stephen.gillham@besweb.com

Tovuti: www.besweb.com
Barua pepe: info@besweb.com

**Mshirika Tanzania (Tanzania Partner)**
World Vision Tanzania
S.L.P. 6070 Arusha, Tanzania
Barua Pepe ya Mawasiliano: david_ombeni@wvi.org
Simu: +255 687 231 757

## MWONGOZO kwa WAALIMU

Mwanzoni, masomo ya Wakati na Biblia yaliandaliwa ili yatumike kwa njia ya posta kukiwepo na kituo cha Shule ya Biblia kwa njia ya posta. Sasa hivi, masomo yanaendelea kutumika kwa wingi hata kwenye sehemu ambazo hazina ufanisi wa kutumia mfumo wa posta au hakuna kabisa mfumo wa posta hasa katika makanisa na shule zilizopo Afrika, India na maeneo mengine. Mwongozo kwa Walimu umeandaliwa kwa wale wanaotumia masomo ya Wakati na Biblia katika hali kama hizo. Mwongozo kwa Walimu katika kitabu hiki umeandaliwa kutumika kwa masomo ya Daraja 0, Daraja la kwanza na Daraja la pili kwa watoto wenye umri kutoka chekechea hadi wastani miaka 10. Masomo ya Daraja 0 hayajajapishwa ila yanaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti ya BES.

Kila Mwongozo wa kufundisha hufuata vifungu vile vile vya Biblia vilivyopo katika somo la Wakati na Biblia. Masomo ya Wakati na Biblia na Mwongozo vimeandaliwa vitumike kila wiki. Masomo ya mwezi Aprili yanahusu Pasaka na masomo ya mwezi Desemba yanahusu Krismasi.

Baadhi ya sehemu watakuwa wanatumia masomo yaliyo katika toleo la A4 la kila wiki na wengine watakuwa wanatumia kitabu cha A5 chenye masomo 24 ndani yake. Kwa kawaida, mwalimu au kiongozi hutoa somo la mwezi toleo la A4 na kila wiki sehemu ya kazi hujazwa kanisani au shuleni au hupelekwa nyumbani na kurejeshwa wiki inayofuatia. Mwishoni mwa mwezi, mwalimu au kiongozi hukusanya somo na kwenda kusahihisha kama inavyotakiwa na kumrudishia mwanafunzi/mtoto kazi iliyosahihishwa mapema iwezekanavyo.

Unapotumia kitabu, mwisho wa kila kipindi, vitabu hukusanywa na kusahihishwa. Tumegundua katika sehemu nyingi kuwa, hili haliwezekani. Hivyo basi, pale darasani masomo yanaweza kugawanywa kwa wanafunzi wengine na mwalimu au kiongozi ataongoza usahihishaji wa somo na wanafunzi watasahihisha masomo ya rafiki zao na kutoa maksi. Nyuma ya kitabu kuna sehemu kwa ajili ya kuweka maksi ya kila somo la mwezi na pia mahali pa maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Pia kuna cheti ambacho mwanafunzi anaweza kupewa kinachoonesha asilimia ya alama ambazo mwanafunzi amepata kwa masomo ya miezi sita.

## MAANDALIZI KWA WAALIMU

Mwongozo huu wa Walimu siyu shinikizo ambao hauwapi walimu fursa ya kufanya mambo kwa njia zao wenyewe kulingana na mawazo na mipango yao wenyewe. Haya ni mapendekezo yanayoweza kutumika kwenye utumiaji wa masomo ya Wakati na Biblia.

- **Elewa habari vizuri** – Walimu wanapaswa kuelewa habari ya Biblia vizuri kwa kadiri iwezekanavyo na vile vile somo la Wakati na Biblia linaloendana na habari hiyo ya Biblia. Ni jambo zuri kwa mwalimu kukamilisha somo la Wakati na Biblia kabla ya kipindi. Mwongozo wa kila somo unapaswa kutumiwa kwa umakini kama chombo cha kumsaidia mwalimu anapojiandaa kwa ajili ya somo.
- **Elewa funzo ambalo watoto wanastahili kupata au kujifunza** – Juu ya kila mpangilio wa somo utaona maneno ‘Tunajifunza kuwa’ ikifuatiwa na makusudio mawili ya kujifunza ambayo tunatumaini kwamba watoto watayaelewa baada ya kumsikiliza mwalimu akifundisha na kukamilisha somo la Wakati na Biblia. Kusudio la kwanza la kujifunza jambo linahusu ufahamu wa habari na la pili linamtia moyo mtoto kufikiri juu ya ufahamu huo, kuutumia na kuuitikia. Makusudio haya ya kujifunza ni sentensi kamilifu na fupi ya mawazo au kweli kuu zinazofundishwa katika somo. Walimu wanaweza kuzitumia kwa ajili ya tathimini zao binafsi za ufundishaji na mafunzo ambayo watoto wamepata.
- **Toa Utangulizi** – Kwa masomo yote, tunaanzia mahali ambapo watoto wapo katika uzoefu wao wa hali husika. Tumependekeza njia kadhaa ambazo zinaweza kutumika kufanya utangulizi wa habari ili kuwawezesha watoto kuhusika katika kujadili mwanzo wa habari.
- **Fundisha** – Tumetoa dondoo muhimu katika habari. Tunaamini kwamba walimu hawatazinukuu wakati wanafundisha habari lakini watakuwa na uelewa mzuri wa habari na wataweza kuifundisha katika njia inayofurahisha na kusisimua. Mwalimu atahitaji watoto waelewe mafunzo muhimu kutoka kwenye habari na kuwasaidia kuuelewa mwitikio watakaoupata kutoka kwenye habari waliyojifunza. Kwa usahihi, tumejaribu kuweka pamoja baadhi ya maelezo kwa ajili ya kufundisha habari. Haya yameandikwa katika maandishi *YA MCHALAZO (Italics)*.
- **Jifunze** – Kuna Mstari Muhimu ambao umewekwa katika kila habari. Katika baadhi ya maeneo, kuna Mistari Muhimu miwili. Mstari huu ulioongezwa unaweza kuwa rahisi kwa watoto kujifunza. Tunatumaini kwamba, watoto watajifunza Mistari muhimu na watakumbushiwa mstari huo mara nyingi iwezekanavyo ili waanze kujenga ufahamu wa Mistari muhimu ya Biblia.

- **Kamilisha** – Katika mazingira ya shule, utatambua uwezo wa watoto kwenye kukamilisha kazi na kiasi cha usaidizi ambao wanauhitaji kutoka kwa mwalimu. Kwa baadhi yao, itahitajika mwalimu asome maandishi katika somo na watoto kufuatilia habari ambayo sasa watakuwa wanaielewa. Watoto wengine wanaweza kusoma maandishi ya somo peke yao. Kwa hali yoyote kati ya zilizotajwa, ni wazo zuri kuwahamasisha watoto wawe makini na kuwapa maelekezo muhimu yanayohusiana na maswali. Kama unatumia masomo ya Wakati na Biblia katika maeneo ambayo siyo shule, ni muhimu walimu kuwepo na kuwasaidia watoto ili wasichukulie masomo haya kama kazi isiyo na mvuto au kama mtihani. Masomo haya yanapaswa kuwa ya kufurahisha na kutia moyo. Ni muhimu kuwasifia watoto wanapoendelea kufanya masomo na kujibu maswali.
- **Kumbuka** – Tunashauri matumizi ya maswali mafupi na maigizo ili kuwasaidia watoto kujifunza na kurudia habari ili kuielewa vyema.
- **Kuonesha** – Tunatambua kuwa katika baadhi ya mazingira, sio rahisi kupata vielelezo au video. Lakini, ni muhimu kadiri iwezekanavyo kuwa na picha au vitu vinavyoweza kuwasaidia watoto kuielewa habari vizuri zaidi. Vielelezo vitakuwa muhimu sana wakati ambapo mwalimu anaelezea habari. Kadiri iwezekanavyo kwenye kila somo, tumetoa maelezo kuhusu picha kutoka kwa picha za www.freebibleimages.org (FBI) ambazo zinaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti yao. Mwisho wa Mwongozo wa Walimu kuna viambatisho vyenye viungo (hyperlinks) vya picha tofauti na zinazofaa kwa kila habari kutoka kwenye tovuti ya Free Bible Images. Kama kuna kinakilishi (photocopier), baadhi ya picha za Bibletime zinaweza kufanywa kuwa kubwa, kupakwa rangi na kutumiwa kufundisha.

## Kupangilia Muda

- **Ratiba –** Tumeweka ratiba sawa kwenye mwongozo wa kufundisha kila somo lakini mwalimu anaruhusiwa kubadilisha ratiba hii mara kwa mara kulingana na mahitaji ya darasa lake/ watoto anaowafundisha.
    1. Utangulizi na kuwaambia watoto habari husika – Takriban dakika 15
    2. Kufundisha Mstari muhimu – dakika 5 hadi10
    3. Kujaza nakala ya somo – dakika 20
    4. Maswali na shughuli zinginezo- dakika 5 hadi10

Kumbuka msemo muhimu:

“Niambie na nitasahau,
Nioneshe na nitakumbuka,
Nihusishe na nitaelewa”

## Mtaala wa Wakati na Biblia

| | **Daraja 0**<br>**(Chekechea/Chini ya miaka mitano)**<br>**Daraja la Kwanza**<br>**(Miaka mitano hadi saba)**<br>**Daraja la Pili**<br>**(Miaka nane hadi kumi)** | **Daraja la Tatu**<br>**(Miaka kumi na mmoja hadi kumi na mitatu)** | **Daraja la Nne**<br>**(Miaka kumi na minne na zaidi)** |
|---|---|---|---|
| **SOMO LA KUANZIA** | Somo la kuanzia – Utangulizi (Inaandaliwa) | Somo la kuanzia – Utangulizi (Inaandaliwa) | Somo la kuanzia – Utangulizi (Inaandaliwa) |
| **MFULULIZO WA A** | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Ibrahimu<br>6. Ibrahimu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa Kwanza<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo na Kuanguka<br>2. Matukio ya Kwanza-Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya Ukristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi |
| **MFULULIZO WA B** | 1. Maisha ya kwanza ya Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Mifano<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Walioandika vitabu vya Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Yusufu<br>8. Matendo ya Mitume 2: 42 – Njia iliyoko mbele<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Amri<br>12. Habari ya Krismasi |
| **MFULULIZO WA C** | 1. Danieli<br>2. Miujiza zaidi<br>3. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu na Samweli<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>3. Miujiza zaidi<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8 Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu ambao Mungu aliwatumia – Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Kristo<br>3. Nguvu za Bwana<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu zaidi wa Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi |

## B7 Habari ya Kwanza

**Kuwasili kwa ndugu zake Yusufu – Habari hii inahusu matokeo ya kufanya vibaya.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Ndoto za Yusufu kuhusu ndugu zake zilitimia.<br>• Mambo mabaya tunayofanya yanatupata mapema au baadaye.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Wagalatia 6: 7***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 42: 1-26*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Wafanye watoto wajadili katika vikundi habari ya Yusufu hadi kufikia hatua hii. Jaribu kutambua mambo mabaya na mazuri ambayo yametokea hadi sasa. Fupisha kwa kusema kuwa mambo yamemwendea vizuri Yusufu licha ya mambo mabaya aliyokuwa ametendewa na ndugu zake. Lakini ndugu zake wanafanya nini huko katika nchi ya Kanaani? Habari hii ya leo inaturudisha Kanaani. |
| **FUNDISHA** | • Kuna wakati katika nchi ya Kanaani watu walikuwa wana njaa. Kulikuwa na njaa na watu hawakuwa na chakula. Yakobo alikuwa amesikia kuwa kulikuwa na chakula kingi kilichohifadhiwa huko Misri. Aliwaambia ndugu zake Yusufu washuke Misri ili kununua chakula kwa ajili ya familia yao. Ndugu wote walienda isipokuwa Benyamini, mdogo wake Yusufu. Waulize watoto kama wanaweza kufahamu kwa nini. ***(Mwanzo 42: 1-5)***<br>• Huko Misri, Yusufu alikuwa msimamizi wa kuuza chakula. Ndugu zake walipofika, wote wakaenda kumsujudia Yusufu, Gavana wa Misri! ***(Mwanzo 42: 6-7)***<br>• *Wakumbushe watoto ndoto alizoota Yusufu kuhusu ndugu zake kabla hawajamuuza. Jadili jinsi ndoto zilivyokuwa zikitimizwa.*<br>• Yusufu alijifanya kuwa hawafahamu ndugu zake nao hawakumtambua. Aliwatendea kama wageni na kusema, ‘Ninyi ni wapelelezi! Mmekuja kuipeleleza nchi!’ Ndugu zake wakamwambia kuwa sio kweli. Walimwambia Yusufu kuwa walikuwa watu waaminifu na wote ni wana wa mtu mmoja. Walimwambia Yusufu kuwa walikuwa na ndugu ambaye ‘alishakufa’ na ndugu mdogo ambaye yuko nyumbani. Ili kujua kama walikuwa wanasema kweli, Yusufu aliwaomba warudi Kaanani wakamchukue ndugu yao mdogo waje nae. Ili kuhakikisha kuwa wanarudi alimweka gerezani kaka yao Simeoni. ***(Mwanzo 42: 8-20)***.<br>• Waulize watoto jinsi ndugu zake Yusufu walivyokuwa wakijisikia. Walijadiliana yaliyokuwa yakitendeka kati yao. Walijua kuwa walikuwa wamemkosea Yusufu kwa miaka mingi iliyopita. *Eleza kuwa sasa walikuwa na hatia, na dhambi zao zilikuwa zimewashika. Rejea* ***Hesabu 32: 23*** *ambayo inasema, "dhambi yenu itawapata hapana budi".*<br>• Walikuwa na hakika kuwa Mungu alikuwa akiwaadhibu kwa jinsi walivyomtendea Yusufu. Yusufu alisikia walichokuwa wakisema. Akajitenga nao akalia. ***(Mwanzo 42: 21-24)***<br>• Yusufu aliamuru watu wake wajaze nafaka kwenye magunia ya ndugu zake. Akaagiza fedha zao zirudishwe kwenye magunia yao na kuwapa chakula cha safari. Ndugu wakawapakia punda zao na kuondoka kurudi kwa baba yao. ***(Mwanzo 42: 25-26)***<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kuwasili kwa ndugu zake Yusufu. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na elezea, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Wagalatia 6: 7***. Wakumbushe watoto kuwa dhambi daima hutuingiza kwenye matatizo. Biblia inasema ni kama kupanda mbegu na kisha, siku moja, kukusanya mazao ya kile tulichopanda. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kujikumbusha habari<br>• Kwa nini hawa ndugu walilazimika kuja Misri?<br>• Ni nani aliyekuwa akiuza nafaka huko Misri?<br>• Je, ndugu zake Yusufu walimtambua?<br>• Yusufu aliwatuhumu ndugu zake kwa kosa gani?<br>• Yusufu alitaka wamlete nani Misri?<br>• Ni ndugu yupi aliwekwa gerezani?<br>• Kwa nini ndugu zake walifikiri kuhusu hayo yote yaliyokuwa yanawapata? |

## <u>B7 Habari ya Pili</u>

**Benyamini na habari mbaya – Habari hii inahusu jinsi dhambi zetu zinavyogundulika.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yusufu bado aliwapenda ndugu zake licha ya yote waliyomtendea.<br>• Mungu anampenda kila mmoja wetu licha ya makosa ambayo tumefanya.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Waefeso 4: 32***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 42: 26-44: 13*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Wafanye watoto wafikirie kuwa wao ni kati ya ndugu wanaoelekea nyumbani Kanaani kutoka Misri. Mna chakula cha kutosha kulisha familia zenu sasa! Unajisikiaje? Sasa, hebu fikiria ukifungua gunia lako na kukuta sio tu nafaka bali pia kuna pesa ulizotumia kulipia! Nani aliziweka hapo? Ilikuwa ni mtego? Je, Gavana wa Misri atafikiri umeiba? Ungewezaje kurudi tena Misri kununua chakula zaidi?<br>Kwa namna nyingine, unaweza kukusanya baadhi ya vifaa (gunia, chakula, na pesa) na uigize hili kwa ajili ya watoto. |
| **FUNDISHA** | • Hivyo ndivyo ilivyotokea kwa ndugu <u>wote</u> wakati wakirudi nyumbani. Saidia watoto kuhoji jinsi ambavyo ndugu walikuwa wanahisi. ***(Mwanzo 42: 26-28)***<br>• Waulize watoto wanadhani kwanini Yusufu alikuwa amerudisha pesa kwenye magunia yao. Wakumbushe watoto kuwa hawa ndugu wamegundua kwamba hili limetokea kwa sababu ya dhambi zao dhidi ya Yusufu.<br>• Walipofika nyumbani, walimwambia baba yao kuhusu kile kilichotokea. Walimwambia kuwa Gavana wa Misri alikuwa amewashutumu kuwa ni wapelelezi. Alitaka wamlete Benyamini. Wakati Yakobo aliposikia haya na kuona kuwa pesa zao ziko kwenye magunia yao, aliogopa. ***(Mwanzo 42: 29-38)*** Je! Unafikiri Yakobo atamwacha Benyamini aende Misri?<br>• Kadri muda ulivyopita, njaa ilizidi kuwa kali. Familia ya Yakobo ilikuwa na njaa tena. Saidia watoto kuelewa tatizo alilokuwa nalo Yakobo. Aliwaambia ndugu zake Yusufu warudi Misri kununua nafaka zaidi. Yuda alimwambia kuwa hawawezi kwenda peke yao lazima waende na Benyamini. Alichukua jukumu la kuhakikisha kuwa Benyamini anakuwa salama. Hakuna kitu ambacho Yakobo angeweza kufanya. Walihitaji chakula. Alikubali kumruhusu Benyamini aende Misri. Aliwaambia ndugu zake wachukue pesa mara mbili na zawadi wapeleke kwa Gavana. ***(Mwanzo 43: 1-14)*** *Unafikiri ndugu walikuwa wanajisikiaje wakati wakiondoka ili wakutane tena na Gavana wa Misri?*<br>• Ndugu walifika Misri na kusimama mbele ya Yusufu. Wakati Yusufu alipoona kuwa Benyamini yuko pamoja nao, aliwaagiza watumishi wake waandae karamu kubwa nyumbani kwake. Alikuwa na Simeoni ambaye ametolewa gerezani. Wakati Yusufu alipofika kwenye karamu ndugu walimpigia tena magoti. Wakumbushe watoto ndoto za Yusufu. Aliwauliza jinsi baba yao alivyokuwa anajisikia na akaongea na Benyamini. Yusufu alihuzunika sana ilibidi aondoke pale. Pamoja na yote yaliyokuwa yamemtokea, bado aliwapenda ndugu zake. Hasa Benyamini, ambaye alikuwa mdogo wake wa tumbo moja. Wakati Yusufu aliporudi, chakula kiliandaliwa, na wakala chakula pamoja. ***(Mwanzo 43: 15-34)***. *Elezea kuwa hata tunapofanya mabaya, Mungu anaendelea kutupenda.*<br>• Asubuhi iliyofuata ndugu waliondoka kwenda Kanaani na magunia yao yaliyojaa nafaka. Wakati huo Yusufu alikuwa amepanga kikombe chake maalum cha fedha kiwekwe kwenye gunia la Benyamini. Yusufu alituma watumishi wake kwenda kutafuta kikombe kwa ndugu zake. Kikombe kilipatikana kwenye gunia la Benyamini! Walilazimika kurudi tena Misri! ***(Mwanzo 44: 1-13)*** Wangejisikiaje sasa? *Je! Watoto wanaweza kubashiri nini kitatokea baadaye?*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Benyamini na habari mbaya. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na elezea, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Waefeso 4: 32***. *Jadili neno 'msamaha'. Waelezee watoto kuwa Mungu anatupenda na yuko tayari kila wakati kutusamehe tunapotubu makosa tuliyofanya.* |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kukumbushia habari.<br>• Ndugu walikuta nini kwenye magunia yao?<br>• Je, Yakobo alitaka Benyamini aende Misri? Kwa nini hakutaka iwe hvyo?<br>• Ni nani aliyekubali kumwangalia Benyamini?<br>• Yusufu alijisikiaje alipomwona Benyamini?<br>• Je, Yusufu bado aliwapenda ndugu zake?<br>• Kikombe kilipatikana katika gunia la nani?<br>• Inamaanisha nini kusamehe?<br>• Je, tunahitaji msamaha kutoka kwa Mungu? Kwa nini? |

## B7 Habari ya Tatu

**Msamaha na habari njema – Habari hii inahusu jinsi tunavyopaswa kusameheana.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yusufu aliwasamehe ndugu zake kwa jinsi walivyomtendea.<br>• Mungu anampenda kila mmoja wetu na anataka kutusamehe makosa yetu ambayo tumefanya.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 45: 8***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 44: 14-45: 28*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Wakumbushe watoto kuhusu ziara za ndugu zake Yusufu huko Misri hadi wakati huu. Kikombe cha fedha cha Yusufu kimepatikana kwenye gunia la Benyamini. Ndugu wanarudi Misri wakiwa na mioyo mizito. Gavana angefanya nini? Je, Benyamini angeuawa au angelazimishwa kubaki kama mtumishi? Je, nini kingetokea kwa baba yao ikiwa wangerudi Kanaani bila Benyamini? |
| **FUNDISHA** | • Ndugu zake walirudi nyumbani kwa Yusufu. Alijifanya kuwa na hasira sana nao kwa kuchukua kikombe chake cha fedha. Yuda akazungumza. Alijua kuwa hali hii mbaya ilikuwa imetokea kwa sababu walikuwa watu wenye hatia. *Elezea neno 'hatia'*. Ndugu walijitolea kuwa watumishi wa Yusufu. Hata hivyo, Yusufu alisema kuwa ni yule tu ambaye kikombe kilikuwa kimepatikana ndani ya gunia lake ndiye angebaki akiwa mtumishi wake. Benyamini angelazimika kubaki! ***(Mwanzo 44: 14-17)***<br>• Yuda alizungumza na Yusufu tena. Alimwambia Yusufu kuwa ikiwa Benyamini hangerudi nyumbani, baba yake angekufa kwa huzuni. Yuda alijitolea kubaki badala ya Benyamini. ***(Mwanzo 44: 18-34)*** *Jadili jinsi hawa ndugu walivyopata badiliko la moyo. Ndugu yule yule ambaye wazo lake lilikuwa kumuuza Yusufu utumwani sasa alikuwa akijitolea kuwa mtumwa mwenyewe! Yusufu aliona jinsi ndugu zake wanavyoishi kila mmoja akimjali mwenzake pamoja na kumjali baba yao.*<br>• Yusufu alijua wakati umefika wa kuwaambia ndugu zake yeye ni nani hasa. Aliomba watu wote watoke chumbani isipokuwa ndugu zake kisha akasema, 'Mimi ni Yusufu.' Jadili jinsi ndugu zake walivyojisikia sasa. Je, Yusufu angetaka kulipiza kisasi? Hata hivyo, Yusufu aliwahakikishia kuwa hii yote imekuwa sehemu ya mpango wa Mungu tangu mwanzo. Mungu alikuwa amemtuma Yusufu kwa ajili yao kwenda Misri ili awe huko kuokoa maisha yao wakati wa njaa. ***(Mwanzo 45: 1-8)***<br>*Jadili ukweli kuwa Yusufu aliwasamehe ndugu zake. Mungu atatusamehe makosa tuliyofanya tunapojutia kwa dhati. Kama Yuda katika habari hii, tunapaswa kutambua kuwa tuna hatia na tuko tayari kukubali kuwajibika kwa mambo mabaya katika maisha yetu.*<br>• Yusufu alijua kuwa bado kulikuwa na miaka mitano mingine ya njaa. Alitaka kuitunza familia yake iwe salama. Akawaambia ndugu zake waende nyumbani wakamweleze baba yao kilichotokea. Kisha walipaswa kubeba vitu vyao vyote na kuja kuishi Misri. ***(Mwanzo 45: 9-28)***<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A - Msamaha na habari njema. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na elezea, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Mwanzo 45: 8***. (Unaweza kutumia tu sehemu ya kwanza ya mstari) Wakumbushe watoto kuwa yote yaliyotokea katika maisha ya Yusufu yalikuwa sehemu ya mpango wa Mungu wa kuokoa familia ya Yakobo wakati wa njaa |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kukumbushia habari.<br>• Ni nini kilipatikana kwenye gunia la Benyamini?<br>• Yusufu alitaka kubaki na nani kama mtumishi wake?<br>• Ni nani aliyejitolea kubaki badala ya Benyamini?<br>• Ni nini kingempata Yakobo kama Benyamini hangerudi nyumbani?<br>• Yusufu alijuaje kwamba ndugu zake wamepata badiliko la moyo?<br>• Je, Yusufu aliwasamehe ndugu zake?<br>• Tunapaswa kufanya nini ili dhambi zetu zisamehewe na Mungu? |

<u>**B7 Habari ya Nne**</u>

**Wakiwa pamoja Misri – Habari hii inahusu mpango wa Mungu kwa maisha yetu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yusufu aliungana tena na baba yake, Yakobo.<br>• Mungu anaweza kuleta mema badala ya mabaya ikiwa tunamwamini kikamilifu<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 50: 20***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 46: 1-34*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu kukutana tena, na kukutana na mtu ambaye hujamwona kwa muda mrefu. Je, hii imewahi kutokea katika familia yako? Wakati fulani watu wanafurahi sana mpaka wanalia kwa furaha!<br>Katika habari ya leo tutasikia juu ya mkutano wa ajabu wa kuungana tena. |
| **FUNDISHA** | • Yakobo (Israeli) na familia yake walipakia vitu vyao. Walikusanya wanyama wao na kuanza safari ya kwenda Misri. Wakiwa njiani walifika mahali paitwapo Beer-sheba ambapo walisimama ili kumtolea Mungu dhabihu. *Elezea kuwa walishukuru sana kuwa Mungu alikuwa akiwatunza!* ***(Mwanzo 46: 1)***<br>• Mungu alizungumza na Yakobo katika ndoto. Alimwambia Yakobo asiogope kwenda kuishi Misri. Huko Misri, Mungu angembariki Yakobo na kuifanya familia yake kuwa taifa kubwa. Aliahidi kuwa atakuwa pamoja na Yakobo. ***(Mwanzo 46: 2-4)***<br>• Jadili jinsi Mungu anavyotimiza ahadi zake siku zote.<br>• Yakobo na familia yake walihama kutoka Beer-sheba na kuja Misri. Walikuwa ni umati mkubwa wa watu! Kwa ujumla, kulikuwa na watu 70 wa familia ya Yakobo huko Misri sasa! ***(Mwanzo 46: 5-27)***<br>• Walipofika wote katika nchi ya Gosheni iliyokuwa sehemu ya Misri, Yusufu akaja kuwalaki. Alifurahi sana kumuona baba yake baada ya miaka mingi sana. Alimkumbatia baba yake na kulia kwa muda mrefu. Mfalme Farao akasikia kuwa wamekuja. Aliwakaribisha na kuwaruhusu kuishi pamoja katika nchi ya Gosheni. ***(Mwanzo 46: 28-34)***<br>• *Jadili mwisho huu mzuri na watoto. Elezea kuwa tunapaswa kumwamini Mungu katika nyakati nzuri na katika nyakati mbaya pia kama vile Yusufu alivyofanya. Tukimtegemea Mungu atatenda mema hata katika hali ngumu ikiwa tunamwamini kikamilifu.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Wakiwa pamoja Misri. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na elezea, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Mwanzo 50: 20***. Tumia mstari huu kuhitimisha habari nzima. Namna gani ndugu walijaribu kumuumiza Yusufu? Jinsi gani, Mungu aligeuza hali hii kuwa nzuri? Hakikisha kuwa watoto wanaelewa kuwa Mungu ndiye anayetawala maisha yetu yote. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kukumbushia habari.<br>• Familia ya Yakobo ilikuwa ikihamia wapi?<br>• Walisimama wapi ili kutoa dhabihu?<br>• Mungu alitoa ahadi gani kwa Yakobo?<br>• Ni nani alikuja kukutana nao walipofika Gosheni?<br>• Ni watu wangapi wa familia ya Yakobo waliokuwa wakiishi Misri sasa?<br>• Mambo ya kuhuzunisha yalitokea katika maisha ya Yusufu. Jinsi gani Mungu alileta mwisho wenye furaha? |

**<u>B8 Habari ya Kwanza</u>**

**Watu ambao Yesu alikutana nao: mwanamke aliyekuwa anaumwa – Habari hii inahusu uwezo wa Bwana Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu aliwaponya watu kwa sababu Yeye ni Mwana wa Mungu.<br>• Bwana Yesu anaweza kufanya mambo mema katika maisha yetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 10: 38***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 4: 38-44*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waambie watoto wasimame na kufanya mazoezi ya mwili “papo kwa papo” - k.m. kuruka, kukimbia taratibu, kukimbia mbio, kuruka kwa mguu mmoja, kutembea, kutumia mikono kupiga hewa mbele yao, au kama muda unaruhusu, wanaweza kucheza mchezo wa taa za barabarani. Unapotaja rangi, watoto hufuata maelekezo - Nyekundu = tulia, Chungwa = kimbia taratibu, Kijani = zunguka. Watoto wanaoshindwa kufuata taa za barabarani wanakuwa nje ya mchezo. Mwishoni elezea kuwa wameweza kufurahia mazoezi haya kwa sababu walikuwa na afya njema. Haifurahishi tunapokuwa wagonjwa na kuwa kitandani. Wakati wa Yesu, kulikuwa na wagonjwa wengi lakini hakukuwa na madaktari wala dawa za kuwasaidia.<br>Kuwa makini kwa watoto wote ambao hawataweza kushiriki katika utangulizi huu. Badala ya maelezo yaliyotangulia unaweza kuzungumza kuhusu ingekuwaje kuwa daktari leo – kujua kuhusu magonjwa mengi, kuagiza matumizi ya dawa, kuwa na shughuli nyingi, wakati mwingine kuweza kusaidia, lakini wakati mwingine kutoweza. Elezea kuwa katika habari ya leo tutajifunza kuhusu daktari wa ajabu kuliko wote - Bwana Yesu! |
| **FUNDISHA** | • Yesu alikuwa katika sinagogi (jengo ambamo Wayahudi walikutana ili kujifunza juu ya Mungu) akiwafundisha watu. Pia alimponya mtu. Sasa ilikuwa wakati wa kutembelea nyumba ya Simoni pamoja na baadhi ya wanafunzi wengine. Lakini kulikuwa na tatizo. Mama mkwe wa Simoni *(elezea hii ina maana gani)* alikuwa mgonjwa sana wa homa. *Elezea jinsi homa ilivyomfanya ajihisi - joto sana na vidonda mwili mzima.* Simoni na wengine walijua kuwa Yesu angeweza kumponya, hivyo wakamwomba Yesu awasaidie. *Kwa nini walifikiri Yesu angeweza kusaidia?* ***(Luka 4: 38)***<br>• Yesu alikuwa tayari kusaidia. Aligusa mkono wa yule mwaname na kukemea homa na kisha akamsaidia kuinuka. Ghafla akapona na kuanza kuwahudumia kwa chakula. Ikama kama vile hakuwahi kuwa mgonjwa! *Waulize watoto kufikiria baadhi ya mambo ambayo watu wanaweza kuwa wameambiana.* ***(Luka 4: 39)***<br>• Jioni hiyo jua lilipokuwa linatua; watu wengi walileta wagonjwa na wenye matatizo kwa Yesu. *Tafakari juu ya aina ya watu ambao waliweza kuwa huko na kwa nini walikuja. Je, inawezekana Yesu alijisikiaje baada ya haya yote? Japo muda ulikuwa umeenda sana, Yesu bado alikuwa na muda wa kuwahudumia watu.* Aliweka mikono Yake juu ya kila mmoja. Hakuna aliyeondoka bila kuponywa. *Tena, jadili kuhusu mwitikio wa watu.* ***(Luka 4: 40-41)***<br>• Asubuhi iliyofuata, Yesu alitafuta mahali pa utulivu ambapo angeweza kusali kwa Baba Yake. Lakini bado watu walikuja kumtafuta! Walijua juu ya uwezo Wake wa ajabu. ***(Luka 4: 42)***<br>• Leo Bwana Yesu bado anajali na anataka kuwasaidia watu. Anaweza kufanya mambo mazuri katika maisha yetu tunapokuwa tayari kumwamini.<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Watu ambao Yesu alikutana nao: mwanamke aliyekuwa anaumwa. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na elezea, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Matendo 10: 38***. Chagua sehemu ya mstari huu kadri kikundi chako kinavyoweza kuukumbuka |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kukumbushia habari<br>• Yesu alikuwa akifanya nini katika sinagogi?<br>• Yesu alitembelea nyumba ya nani?<br>• Nani alikuwa na homa?<br>• Yesu alifanya mambo gani mawili kumponya?<br>• Alifanya nini baada ya kuponywa?<br>• Kwa nini watu wengi zaidi waliendelea kuja kwa Yesu?<br>• Yesu alifanya jambo gani muhimu asubuhi iliyofuata?<br>• Jaza neno linalokosekana, “Yesu alizunguka huko na huko akitenda _______.” |

## B8 Habari ya Pili

**Watu ambao Yesu alikutana nao: mtu mwenye ukoma – Habari hii inahusu jinsi Bwana Yesu anavyotupend.**

**Tunajifunza kuwa:**
- Yesu alionyesha upendo wake kwa kumponya mtu mwenye ukoma.
- Yesu anatupenda na anataka kubadilisha maisha yetu.

**Mstari Muhimu:** ***Luka 7: 22***
**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 5: 12-16***

### TOA UTANGULIZI

Waulize watoto kuhusu magonjwa ya kuambukiza ambayo wana uzoefu nayo, k.m. tetekuwanga, surua. Zungumza kuhusu kulazimika kukaa mbali na wengine na kushindwa kufanya shughuli za kawaida. Elezea kuwa wakati wa Yesu, ukoma ulikuwa ugonjwa wa ngozi ambao ulisambaa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Watu waliopatwa na ukoma hawakuweza tena kuishi na familia zao au kwenda kazini. Haikuwepo tiba!
Himiza kikundi kushukuru kwa kiwango chochote cha huduma ya afya kinachopatikana - labda unaweza kueleza kuhusu hili kwa njia ya maombi.

### FUNDISHA

- Siku moja, mtu mwenye ukoma mbaya sana alimkaribia Yesu. Alipiga magoti mbele ya Yesu na kuomba msaada. Akasema, "Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa." Hilo lilionyesha kuwa mtu huyo alijua kuwa Yesu alikuwa na uwezo wa kumtakasa ikiwa yuko tayari kufanya hivyo. Bashiri juu ya kile ambacho Yesu anaweza kufanya. Je, Yesu angetaka kujihusisha kwa namna yoyote na mtu aliyekuwa na ugonjwa wa kuambukiza? Je, atakuwa tayari kumfanya mtu huyo awe mzima? ***(Luka 5: 12)***
- Bila shaka, Yesu alitaka kumsaidia mtu huyo. Alimpenda sana na alijua ni kiasi gani alihitaji msaada. Kisha Yesu akafanya jambo la ajabu. Alinyoosha mkono Wake na akamgusa mtu huyo na kusema, "Nataka; takasika!" Yesu hakupata ukoma kwa kumgusa mtu huyo lakini badala yake mtu huyo akapona mara moja. *Elezea jinsi ngozi yake ilivyokuwa nyororo na yenye afya; pia tafakari juu ya mshangao na shukrani ya mtu huyo.* ***(Luka 5: 13)***
  *Huu ulikuwa muujiza mwingine. Yesu alikuwa ameonyesha tena uwezo wake mkuu juu ya ugonjwa na kubadilisha maisha ya watu.*
- Biblia inalinganisha dhambi zetu na ukoma. Zungumza kuhusu dhambi ni nini na jinsi inavyoharibu maisha yetu. Yesu, ambaye hakuwa na dhambi alikuwa tayari kuja duniani ili kutuokoa sisi sote, wenye dhambi. Anatupenda licha ya mambo mabaya ambayo tumefanya. Ikiwa tuko tayari, anaweza kutusamehe na kutusafisha dhambi zetu. Maisha yetu yanaweza kubadilishwa kwa ndani.
- Baada ya Yesu kumponya mtu huyo, alimwambia aende akajionyeshe kwa kuhani kuwa amepona. *Jinsi gani maisha yake yangekuwa tofauti kuanzia sasa?* Mtu huyo hangesahau kamwe siku aliyokutana na Yesu. ***(Luka 5: 14)*** Tukimwomba Bwana Yesu atusamehe dhambi zetu, itakuwa siku bora zaidi maishani mwetu pia.

**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**

**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A - Watu ambao Yesu alikutana nao: mtu mwenye ukoma.

### JIFUNZE

Fundisha na elezea, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Luka 7: 22***. Mstari huu unaorodhesha njia sita ambazo Bwana Yesu anazitumia kubadilisha maisha ya watu. Kuzipangilia zote inaweza kuwa changamoto - jaribu kutumia maigizo rahisi yasiyo na matamshi kwa kila kifungu cha maneno k.m. vipofu=nyoosha kwenye macho, viwete tembea= tembea hapohapo, wenye ukoma = kugusa ngozi kwenye kiganja cha mikono. Vinginevyo, gawanya katika vishazi kwa vikundi tofauti waviseme kama ni ndefu sana. Watoto wa daraja la pili wenye ujuzi mzuri wa Biblia wanaweza kujaribu kutoa mifano maalum ya watu ambao Yesu aliwaponya kutoka katika kila kundi.

### KUMBUKA

Jibu kweli au si kweli katika sentensi za jaribio hili.
- Ukoma ni ugonjwa wa kuambukiza.
- Huyu mtu aliruhusiwa kuwa na familia yake tu.
- Alipiga magoti mbele ya Yesu.
- Huyu mtu hakuwa na uhakika kama Yesu angeweza kumponya
- Yesu alimgusa.
- Yesu aliweza kumponya kwa sababu Yeye ni Mwana wa Mungu.
- Alipona baada ya dakika chache.
- Alilazimika kwenda kujionyesha kwa kuhani.
- Sisi sote tuna ugonjwa unaoitwa dhambi.
- Bwana Yesu anatupenda na yuko tayari kutusamehe dhambi zetu.

**B8 Habari ya Tatu**

**Watu ambao Yesu alikutana nao: mtu mwenye kupooza – Habari hii inahusu jinsi Bwana Yesu anavyosamehe.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu alikuwa na uwezo sio tu wa kuponya mtu aliyepooza bali pia kusamehe dhambi zake.<br>• Yesu ana uwezo wa kusamehe dhambi zetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 5: 24***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 5: 17-26*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize watoto wapendekeze mambo ambayo wanaweza kufanya ili kumsaidia rafiki shuleni au nyumbani. Pongeza kujitoa kwao kusaidia. Katika habari ya leo, marafiki wanne walimbeba rafiki yao ambaye hawezi kutembea, wakampeleka kwa Yesu. Ikiwezekana, uwe na mkeka kama nyenzo ya kueleza jinsi walivyofanya jambo hilo. Kwa nini walimleta kwa Yesu? Ndiyo, walijua kuwa Yesu alikuwa na uwezo wa kumponya rafiki yao. |
| **FUNDISHA** | • Hata hivyo, kufika alipokuwa Yesu haikuwa rahisi kama walivyotarajia. Watu wengi walikuwa tayari wamejazana ndani ya nyumba kumsikiliza Yesu. Ni muhimu kwetu pia kutaka kusikiliza maneno ya Yesu. Haikuwezekana kupita mlangoni, kwa hiyo wakambeba mtu huyo wakampandisha kwenye ngazi za kando ya nyumba hadi kwenye paa. Wasingekata tamaa kirahisi kwa sababu walijua kuwa Yesu pekee ndiye angeweza kusaidia! *Waombe watoto wafikirie jinsi ilivyokuwa kwa watu waliosimama chini ya nyumba wakati shimo lilipotokea kwenye paa na mtu huyo akashushwa kwa uangalifu mbele ya miguu ya Yesu.* ***(Luka 5: 18-19)***<br>• *Yesu angemponyaje mtu huyo? Waulize watoto kukumbuka jinsi alivyoponya katika habari za mama mkwe wa Petro na mwenye ukoma.* Lakini habari ya leo, Yesu alizungumza na mtu huyo na kumwambia, "Ee rafiki, umesamehewa dhambi zako." Baadhi ya watu waliokuwa ndani ya nyumba hiyo walikasirika. Hawakuamini kuwa Yesu angeweza kusamehe dhambi. Walidhani kuwa ni Mungu pekee ndiye anayeweza kusamehe dhambi na hawakuamini kuwa Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Yesu alijua walichokuwa wakifikiri. *Anajua mawazo yetu pia!* ***(Luka 5: 20-24)***<br>• Yesu alitaka kuwathibitishia kuwa kweli alikuwa amesamehe dhambi za mtu huyo ingawa hawakuweza kuona maisha ya mtu huyo! Kwa hiyo, Alimwambia yule mtu aliyepooza ainuke, achukue mkeka wake na aende nyumbani. Mara yule mtu akafanya hivyo, akaenda zake huku akimtukuza Mungu! Kila mtu alishangaa. Nguvu za Yesu hazikuponya tu miguu ya mtu huyo, bali aliweza pia kusamehe dhambi! Hakuna mtu mwingine aliyekuwa na nguvu kama hii! ***(Luka 5: 24-26)***<br>• Hitaji letu kuu ni kusamehewa dhambi zetu. *Rejea kile watoto walichojifunza katika Habari ya Pili – dhambi ni nini, jinsi inavyoharibu uhusiano wetu na Mungu na kutukosesha Mbingu.* Bwana Yesu anao uwezo wa kutusamehe dhambi zetu kwa sababu Yeye mwenyewe hakuwa na dhambi. Alikuwa tayari kufa msalabani kuchukua adhabu ya dhambi zetu. Tunahitaji kujutia dhambi zetu kwelikweli na kumshukuru Bwana Yesu kwa kutupa njia ya kusamehewa.<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A - Watu ambao Yesu alikutana nao: mtu mwenye kupooza. |
| **JIFUNZE** | Fundisha Mstari Muhimu ambao ni sehemu ya habari. ***Luka 5: 24***. Elezea kuwa “Mwana wa Adamu” ni jina jingine la Bwana Yesu. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kukumbushia habari<br>• Mtu huyo alikuwa na marafiki wangapi?<br>• Je, mtu huyo alikuwa na tatizo gani?<br>• Kwa nini ilikuwa vigumu kumpeleka rafiki yao kwa Yesu?<br>• Waliingiaje ndani ya nyumba?<br>• Jambo gani la kwanza Yesu alimwambia mtu huyo?<br>• Kwa nini baadhi ya watu walikuwa na hasira?<br>• Yesu alionesha jinsi gani alikuwa amesamehe dhambi za mtu huyo?<br>• Ni jambo gani la muhimu zaidi ambalo Bwana Yesu anaweza kutufanyia? |

## B8 Habari ya Nne

**Watu ambao Yesu alikutana nao: Mathayo – Habari hii inahusu kumfuata Bwana Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu alijua maisha ya Mathayo yalikuwaje, lakini bado alimtaka amfuate.<br>• Yesu anataka tumfuate.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 5: 32***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 5: 27-32*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Kuwa na majadiliano na watoto kuhusu aina za kazi ambazo wangependa kufanya watakapokuwa wakubwa. Tathmini nini kingefaa katika kufanya kazi hizi.<br>Au<br>Fanya maigizo rahisi ya kazi za kawaida katika jamii yako ili watoto waweze kukisia wao ni nani. Elezea kuwa habari ya leo inamhusu mtu anayeitwa Mathayo (Lawi) ambaye alikuwa mtoza ushuru. Aliketi kando ya barabara na kukusanya ushuru kutoka kwa watu na kuwapelekea Warumi waliokuwa wasimamizi wa nchi. Unaweza kurejea ukweli kwamba bado tunalipa ushuru leo na kuwa ushuru huo unatumikaje.<br>Kwa bahati mbaya, hakuna mtu aliyempenda Mathayo. Watoza-ushuru hawakupendwa sio tu kwa sababu walifanya kazi kwa ajili ya adui (Warumi) bali pia kwa sababu wakati fulani walichukua pesa nyingi kuliko walizopaswa na kuzichukua kwa ajili yao binafsi. |
| **FUNDISHA** | • Siku moja Yesu alimwona Mathayo akifanya kazi yake. *Tafakari juu ya kile Yesu alichofikiri kuhusu Mathayo - Je! Alijua Mathayo alikuwa mtu wa aina gani? Ndiyo bila shaka ...Anajua kila kitu kuhusu kila mmoja wetu. Je, Yesu angetaka kufanya chochote pamoja na Mathayo? Ndiyo! Mathayo alikuwa ni mmoja wa watu ambao Yesu alikuja kuwasaidia - Angeweza kubadilisha maisha ya Mathayo!* Kwa hiyo, Alisimama kando ya Mathayo na kusema, *“Nifuate.”* ***(Luka 5: 27)*** *Mathayo alifanya nini? Onesha chaguo ambalo Mathayo alipaswa kufanya.*<br>• Mathayo alijua mara moja alichotakiwa kufanya. Alitakiwa kumfuata Yesu! Ni ajabu kiasi gani kwamba Yesu alikuwa amemwalika! Akainuka, akaacha kila kitu, akaenda pamoja na Yesu. ***(Luka 5: 28)*** *Elezea kuwa Bwana Yesu anampa kila mmoja wetu mwaliko wa kumfuata na kuwa Naye katika maisha yetu. Sisi pia tunahitaji kufanya uchaguzi.*<br>Mathayo alitaka marafiki zake wakutane na Yesu na kuwajulisha jinsi maisha yake yalivyokuwa yamebadilika. Basi, akawaalika pamoja na Yesu na wanafunzi wake kwenye chakula cha jioni nyumbani kwake. Baadhi ya watu waliokuwa pale walifikiri kuwa Yesu alikosea kuchanganyika na Mathayo na marafiki zake. Walifikiri kuwa Yesu alipaswa kutumia muda na watu wema badala ya wenye dhambi. Hawakutambua kuwa kila mtu ni mwenye dhambi. Yesu aliwaeleza kwa nini alikuja duniani – si kwa ajili ya watu waliodhani maisha yao yalikuwa mazuri bali kwa wale waliojua kuwa wametenda dhambi na walitaka kujutia dhambi zao. ***(Luka 5: 29-32)***<br>Yesu hapendi dhambi, lakini anawapenda wenye dhambi kama Mathayo na sisi! Sisi pia tunahitaji kumfuata na kumwamini kwa ajili ya msamaha.<br>• Baadaye, Mungu alimchagua Mathayo kufanya kazi muhimu sana. Aliandika kitabu cha kwanza cha Agano Jipya. Ilikuwa siku ya pekee sana alipoamua kumfuata Yesu na kumruhusu Yesu ashughulikie mambo mabaya maishani mwake. Tangu wakati huo, maisha yake yalibadilika.<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A - Watu ambao Yesu alikutana nao: Mathayo. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na elezea, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Luka 5: 32***. Kuelezea maneno yote magumu - k.m. haki na toba. |
| **KUMBUKA** | Katika mazingira ya darasani, watoto wangeweza kutengeneza jedwali linalojumuisha picha za watu mbalimbali ambao Yesu alikutana nao katika habari hizi. Au unaweza kuwa na zoezi la kurejea kulingana na B8 yote, ukitumia maswali yaliyochaguliwa kutoka kwa vidokezo vilivyotangulia na machache kuhusu Mathayo mf<br>• Kazi ya Mathayo ilikuwa nini?<br>• Yesu alimwambia nini Mathayo?<br>• Mathayo alifanya nini baada ya kumfuata Yesu? |

## B9 Habari ya Kwanza

**Kuzaliwa kwa Musa – Habari hii inahusu Mungu anavyojali.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alimjali Musa na anatujali sisi pia. (Daraja la 1)<br>• Mungu alikuwa na mpango kwa ajili ya maisha ya Musa, kama alivyo na mpango na sisi pia. (Daraja la 2)<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Waebrania 11: 23***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Kutoka 2: 1-10*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Anza kwa kurejelea mpango ambao watoto wanaweza kuuelewa - k.m. mpango wa shule kwa siku, ambapo shughuli hutokea kwa utaratibu fulani. Eleza kwamba Mungu ana mpango kwa ajili ya maisha ya kila mmoja wetu. Familia tunazotoka na mambo yanayotupata si ya kubahatisha - badala yake, Mungu anayatumia kututayarisha ili tumtumikie. Katika habari hizi tutajifunza kuhusu Musa. Mungu alikuwa na kazi muhimu sana ambayo Musa angeifanya atakapokuwa mtu mzima. Leo tutajifunza jinsi Mungu alivyomtunza Musa alipokuwa mtoto. Habari ya Musa inapatikana katika kitabu cha pili cha Biblia. *Uliza kama kuna yeyote anayejua jina la kitabu hiki na waoneshe kilipo.* Vinginevyo, ikiwa unatoa utangulizi wa habari hii kwa watoto wa Daraja la 1, unaweza kuzungumza kuhusu watoto wachanga na ikiwezekana uwe na baadhi ya vitu wanavyohitaji ili kuwaweka salama na katika utulivu. |
| **FUNDISHA** | • Eleza kwa ufupi historia ya Waisraeli (Waebrania) kuwa watumwa - tazama utangulizi wa somo la Daraja la 2. ***(Kutoka 1: 1-11)*** Mfalme Farao alitamani sana kuzuia Waisraeli wasiongezeke kiidadi kiasi kwamba aliamua kuwazamisha watoto wote wa kiume ambao ni Waisraeli katika Mto Nile. ***(Kutoka 1: 22)*** *Mama na baba Mwisraeli walijisikiaje walipopata mtoto wa kiume?*<br>• Katika nyumba moja, mtoto mzuri wa kiume mwenye afya alizaliwa. Wazazi wake walimficha ndani ya nyumba, wakitumaini kwamba Mungu atamlinda. Lakini baada ya miezi mitatu, hawakuweza tena kumficha. *Kwa nini haikuwezekana?* Mama yake alitengeneza kisafina cha manyasi kisichoingia maji *(eleza)*, akamtia mtoto ndani na kuficha kisafina kwenye matete marefu kwenye ukingo wa mto. Miriamu, dada wa mtoto alipewa kazi ya kuangalia kitakachotokea, lakini Mungu pekee ndiye angeweza kumhifadhi mtoto huyo awe salama. ***(Kutoka 2: 1-4)***<br>• Eleza sehemu inayofuata ya habari kwa kuigiza - eleza jinsi Miriamu alivyomuona binti mfalme (binti Farao) na wasaidizi wake wakija. Je, atamuona mtoto? Je, atamwambia mfalme? Ndio, binti mfalme aliona kisafina na akamwomba msaidizi wake amletee. Eleza jibu lake alipomwona mtoto wa Kiebrania ndani. Binti mfalme asingemruhusu adhuriwe! Mungu alikuwa kazini kumhifadhi mtoto awe salama! ***(Kutoka 2: 5-6)***<br>• Kisha Miriam akasogea mbele na kujitolea kutafuta mlezi kwa ajili ya mtoto. *Angempata nani?* Binti mfalme alikubali na Miriamu akakimbia kumtafuta mama yake! Kwa hiyo, mama wa mtoto aliweza kumtunza nyumbani kwa usalama kamili kwa sababu binti mfalme alikubali. Baadaye, mtoto huyo alipokua na kuwa mvulana, binti mfalme alimchukua akaishi katika jumba la kifalme la Farao. Alimchukua na kumwita Musa, maana yake “nalimtoa majini”. ***(Kutoka 2: 7-10)*** Sasa Musa akawa mtoto wa mfalme wa Misri!<br>• *Wasaidie watoto kuelewa kwamba Mungu alikuwa nyuma ya yote yaliyotokea. Kulingana na sheria ya Farao, mtoto alipaswa kufa maji. Wazazi wa Musa walikuwa na imani katika Mungu - walimwamini Mungu kwamba atamtunza mtoto wao na kweli Mungu alifanya hivyo. Huu ulikuwa ni mwanzo tu wa kutimizwa kwa mpango wa Mungu. Mungu anatutaka tumwamini Yeye atimize mpango wake katika maisha yetu.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kuzaliwa kwa Musa / Kuzaliwa kwa Musa. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Waebrania 11: 23*** (Daraja la 2). Watoto wa Darajaj la 1 wanaweza kujifunza sentensi ya kwanza. |
| **KUMBUKA** | • Habari ya Musa inapatikana katika kitabu gani?<br>• Farao aliamua kuwafanyia nini watoto wote wa kiume wa Kiebrania?<br>• Mtoto alifichwa nyumbani kwa muda gani?<br>• Mama alitengeneza nini?<br>• Alimweka mtoto wapi?<br>• Nani alibaki mtoni kutazama?<br>• Ni nani alimuona mtoto?<br>• Kwa nini maisha ya Musa hayakuwa hatarini tangu wakati huo na kuendelea?<br>• Ni nani walioonesha imani katika habari hii?<br>• Ni nani alimlinda Musa? |

## <u>B9 Habari ya Pili</u>

**Kosa kubwa la Musa – Habari hii inahusu kufanya jambo tunalodhani ni bora.**

<table>
<tr><td></td><td>Tunajifunza kuwa:<br>• Musa alifanya makosa alipotenda kwa haraka sana akiwa na hasira.<br>• Hatuwezi kuepuka matokeo ya kufanya mambo mabaya.<br><br>Mstari Muhimu: Kutoka 2: 11-15<br>Habari kwenye Biblia: Hesabu 32: 23</td></tr>
<tr><td>TOA UTANGULIZI</td><td>Wakati mwingine tunadhani kwamba tunajua vyema. Chagua mfano wa kitu ambacho mtoto anaweza kuoneshwa na mtu mzima jinsi ya kukifanya, lakini mtoto hafuati maelekezo na matokeo yake hakifanyi vizuri! Wiki iliyopita tulijifunza kuhusu Musa. Uliza baadhi ya maswali ili kurejea. Musa alienda kuishi wapi alipokuwa mvulana? Watu wake waliitwaje? (Waisraeli/Waebrania). Wakumbushe watoto kwamba walikuwa watumwa na jinsi walivyotendewa kikatili na Wamisri. Katika habari ya leo Musa ni mtu mzima. Sikiliza kwa umakini ili ujifunze kuhusu hali ambayo Musa alidhani anajua vyema.</td></tr>
<tr><td>FUNDISHA</td><td>• Siku moja Musa alienda kuwatembelea watu wake. Ghafla aliona mmoja wao akipigwa na Mmisri. Musa alijisikiaje? (hasira, akitaka kuwatetea watu wake). Kwa haraka Musa akatazama huku na huku na kuona hakuna mtu anayemtazama na akamuua yule mtu kutoka Misri. Kisha akauficha mwili huo kwenye mchanga. Musa alifikiri kuwa amefanya jambo jema lakini je ni kweli! Wawezeshe watoto kuona kwamba kitendo cha Musa kilikuwa kibaya sana. (Daraja la 2: Unaweza pia kutoa maoni jinsi Mungu alivyoliona kosa la Mmisri na kurejelea jinsi Mungu atakavyoshughulikia makosa yote katika siku zijazo.) Je, unafikiri Musa ataepuka madhara ya kile alichokifanya? Ikiwa sivyo, kwa nini? (Kutoka 2: 11-12)<br>• Siku iliyofuata Musa aliwaona Waebrania wawili wakipigana. Alipouliza kinachoendelea, mmoja wa wale watu akasema, “Ni nani aliyekuweka wewe kuwa mwamuzi juu yetu? Je! Wataka kuniua kama ulivyomwua yule Mmisri?” Sasa Musa akajua kwamba alionekana akimwua yule Mmisri. Angejisikiaje sasa? (kuogopa kwamba mfalme atasikia kuhusu jambo hilo) Punde Farao alisikia juu ya kile Musa alichofanya na akataka kumuua. Musa alilazimika kukimbia ili kuokoa maisha yake hadi nchi nyingine iitwayo Midiani ambako alifanya kazi kama mchungaji wa mtu aliyeitwa Yethro. (Kutoka 2: 13-22)<br>• Mungu pia alijua kuhusu jambo baya ambalo Musa alikuwa amefanya. Zungumza jinsi Mungu anavyoona kila jambo tunalofanya, na hatuwezi kumficha makosa yetu. Ingawa Musa alikuwa mtu mzima, alifanya makosa na hakufanya jambo sahihi. Bado alikuwa na mengi ya kujifunza kabla hajawa tayari kuwa kiongozi. Tunahitaji kujifunza kutokana na kosa la Musa na kumtegemea Mungu atusaidie kutenda kwa njia ifaayo ambayo inampendeza.<br><br>Kamilisha somo la Wakati na Biblia.<br><br>Onesha: Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kosa kubwa la Musa.</td></tr>
<tr><td>JIFUNZE</td><td>Fundisha na ueleze, inapobidi, Mstari Muhimu. Hesabu 32: 23 Linganisha mstari huo na kosa la Musa. Dhambi ya Musa ilikuwa nini? Aligundulikaje? Unaweza pia kutoa mfano maalum wa hali ya kugundulika, ambao unaweza kueleweka kwa watoto.</td></tr>
<tr><td>KUMBUKA</td><td>Jibu kweli au si kweli katika sentensi za jaribio hili.<br>• Musa alimuua Mwisraeli.<br>• Alidhani hakuna mtu aliyemwona.<br>• Mwanaume mwingine Mwebrania alikuwa amemwona.<br>• Mungu aliona kilichotokea.<br>• Farao alimtia Musa gerezani.<br>• Musa bado alikuwa na mengi ya kujifunza kabla hajawa tayari kuwa kiongozi.</td></tr>
</table>

## B9 Habari ya Tatu

**Musa aona kijiti kikiwaka moto: Habari hii inahusu kuwa tayari kumtumikia Mungu.**

**Tunajifunza kuwa:**

- Musa alikuwa kiongozi mwenye kusitasita, lakini Mungu aliahidi kumsaidia.
- Mungu ni mtakatifu na tunahitaji kukumbuka hili kila wakati.

**Mstari Muhimu:** ***Kutoka 3: 12***
**Habari kwenye Biblia:** ***Kutoka 3-4: 17***

### TOA UTANGULIZI

Zungumza kuhusu kuombwa kufanya jambo muhimu na la kusisimua, k.m. jukumu muhimu kwa watoto katika kikundi chako. Ulijisikiaje ulipoambiwa kufanya hivyo? (wasiwasi / kutamani angeambiwa mtu mwingine?)
Habari ya leo inatokea miaka 40 baada ya kosa kubwa la Musa. Musa alikuwa mchungaji kwa miaka 40 jangwani. Mungu hakuwa amemsahau. Alikuwa tayari kumsamehe na sasa alikuwa na kazi ya pekee sana aliyotaka aifanye.

### FUNDISHA

- Siku zote zilifanana, hadi siku moja ... Musa alipoona kijiti kinawaka moto. Ajabu ni kwamba ingawa kulikuwa na miali ya moto, majani na matawi hayakuungua! Musa akasogea karibu kutazama na kisha Mungu akataja jina la Musa. *Tumia maneno kutoka katika Biblia kuelezea sehemu inayofuata. Eleza kwamba "nchi takatifu" ilimaanisha kwamba palikuwa mahali pa pekee sana kwa sababu Mungu alikuwa hapo. Tunapaswa kuelewa kwamba Mungu ni mtakatifu na yuko tofauti na sisi. Tofauti na sisi, Mungu hana dhambi.* Musa alivua viatu vyake na kuficha uso wake kwa sababu alielewa ukuu wa Mungu. ***(Kutoka 3: 1-6)***
- *Wasaidie watoto wakumbuke jinsi maisha ya Waisraeli yalivyokuwa huko Misri.* Mungu alimwambia Musa kwamba alijua mambo yote mabaya yaliyokuwa yakitukia na sasa alitaka kuwatoa Misri na kuwapeleka katika nchi mpya. Mungu alitaka Musa awe kiongozi wao na aende kuongea na mfalme Farao. *Tafakari jinsi Musa alivyojisikia kuhusu kurudi kwa Farao.* ***(Kutoka 3: 7-10)***
- *Husianisha kati ya majibu ya kibinafsi ya watoto katika utangulizi na ubashiri wowote sahihi ambao waliufanya kuhusiana na jinsi Musa alivyohisi kuhusu kuwa kiongozi. Kisha husianisha kukataa kwa Musa na majibu ya Mungu kama ilivyoelezewa katika maandiko ya Biblia na katika viputo vya gumzo katika somo la Daraja la 2.* Kwa Daraja la 2, unaweza kutaka kuvirekodi katika safu wima mbili kwenye ubao au chati mgeuzo.
- Sina uwezo wa kutosha - Nitakuwa na wewe. ***(3: 11, 12)*** - Sijui jina lako - Jina langu ni MIMI NIKO AMBAYE NIKO (jina hili linaonyesha kwamba Mungu ni mweza yote). Mimi ni Mungu wa baba zako, Mungu wa Ibrahimu ***(3: 13-15)*** Hawataniamini - Nitakupa miujiza ili kuthibitisha uwezo wangu. ***(4: 1-9)*** Sitaweza kusema maneno sahihi - Nitakusaidia kuzungumza na kukufundisha la kusema. ***(4: 10-12)*** Tafadhali tuma mtu mwingine. ***(4: 13)*** - Haruni atakuwa msaidizi wako na unaweza kumwambia la kusema.
  *Je, Musa alikuwa aina ya mtu ambaye ungetarajia kuwa kiongozi? Je, unafikiri Mungu alifurahishwa na visingizio vyake? Hapana!* Lakini licha ya kosa alilofanya huko Misri na visingizio vyake vyote, alikuwa chaguo la Mungu. Katika habari yetu inayofuata tutajifunza jinsi ambavyo mwishowe Musa alikuwa tayari kutii na Mungu aliweza kuendelea kutekeleza mpango wake katika maisha yake. Musa alipaswa kumtegemea Mungu kwa yote yaliyokuwa mbele yake.
- *Wakati fulani Mungu hutuambia tumfanyie mambo ambayo yanaonekana kuwa magumu. Tunahitaji kukumbuka kwamba yuko pamoja nasi na atatusaidia.*

**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**

**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Musa aona kijiti kikiwaka moto.

### JIFUNZE

Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Kutoka 3: 12a***. Huu ni mstari mfupi baada ya habari ndefu. Watoto wanaweza kupenda kuuandika kwenye vitabu vyao binafsi vya alama au kutengeneza mkusanyiko wa picha (kolagi ya kikundi) huku kila mtoto akipamba au kubandika vipande vya karatasi kwenye herufi.

### KUMBUKA

- Nini kilikuwa cha ajabu kuhusu kijiti ambacho Musa alikiona?
- Musa alifanya nini alipokuwa kwenye ardhi takatifu?
- Utakatifu unamaanisha nini?
- Mungu alitaka Musa afanye kazi gani?
- Taja udhuru ambao Musa alitoa kuhusu yeye mwenyewe.
- Musa alitoa udhuru gani kuhusu Mungu?
- Mungu alimruhusu Musa aende na nani?
- Mungu hakukata tamaa na Musa. Kwa nini haikuwa hivyo?

**<u>B9 Habari ya Nne</u>**

**Musa aleta ujumbe wa Mungu: Habari hii inahusu Musa kurudi Misri.**

**Tunajifunza kuwa:**
- Musa hatimaye alikuwa mtiifu kwa kile ambacho Mungu alimwomba afanye.
- Mungu alitimiza ahadi yake kwa Musa na atafanya vivyo hivyo kwetu sisi pia.

**Mstari Muhimu:** ***Kutoka 4: 15b***
**Habari kwenye Biblia:** ***Kutoka 4: 1-31***

**TOA UTANGULIZI**

Zungumza kuhusu mabadiliko muhimu katika maisha yetu - k.m. kuhamia nyumba mpya, kuhamia shule ya upili, kuoa au kuolewa. Musa alikuwa na mabadiliko mengi katika maisha yake - kumbuka miezi yake ya kwanza akiwa mtoto mchanga, kisha akaishi katika jumba la kifalme la Farao hadi alipokuwa na umri wa miaka 40, ikifuatiwa na maisha yake jangwani kwa miaka 40 nyingine. (Katika mazingira ya darasani ingefaa kuweka picha za matukio haya kwenye mtiririko wa ratiba ya maisha ya Musa.) Sasa Musa alikuwa akikabiliana na changamoto kubwa zaidi maishani mwake. Mungu alikuwa amemtaka afanye nini?

**FUNDISHA**

- Sasa Musa alikuwa na mke na wana wawili katika nchi ya Midiani. Alimwomba baba-mkwe wake, Yethro, kama angeweza kurudi Misri. Yethro alikubali na Musa akaondoka pamoja na mke wake na wanawe wakapanda punda. Musa pia alichukua fimbo yake maalum ambayo Mungu alimwambia aitumie. Mungu alimwambia Musa kwamba watu waliotaka kumuua alipokuwa Misri mara ya mwisho hawakuwa hai tena. Mungu alikuwa akimsaidia Musa asiogope. Tayari Mungu alikuwa anatimiza ahadi yake kwa Musa. *Je, unaweza kukumbuka mstari muhimu wa wiki iliyopita?* ***(Kutoka 4: 18-20)***
- Kisha Mungu akatimiza ahadi nyingine aliyokuwa amempa Musa. Musa alipokuwa bado katika safari yake, ndugu yake Haruni akaja na kukutana naye. *Kwa nini Haruni alikuwa na Musa?* Musa alimwambia Haruni yote ambayo Mungu alikuwa amemwambia, ikijumuisha ishara alizopewa kufanya kwa fimbo yake. *Mungu anaweza kutegemewa sikuzote kutimiza ahadi zake. Ikiwa sisi ni watu wake, atatufanyia vivyo hivyo.* ***(Kutoka 4: 27-28)***
- Walipofika Misri, Musa na Haruni walikutana na viongozi wa Waisraeli na kuwaambia mipango ya Mungu. Kisha watu wote wakakusanyika, na Musa akawaonyesha miujiza ambayo Mungu alimpa afanye kwa fimbo yake. Musa akaitupa ile fimbo chini na ikawa nyoka na kisha aliposhika mkia wa nyoka ikawa fimbo tena. Kisha, aliingiza mkono wake kifuani pake na alipoutoa nje ulikuwa umejaa ukoma *(elezea)* lakini alipoingiza mara ya pili ukapona. ***(Kutoka 4: 6-9)*** Watu walipoona mambo hayo ya ajabu, waliweza kuona nguvu za Mungu, na kuelewa kwamba kwa kweli Musa alikuwa ametumwa na Mungu. Unafikiri watu walijisikiaje? (walishangaa / walikuwa na furaha sana kwamba Mungu alikuwa anaenda kuwaokoa kutoka katika utumwa.) ***(Kutoka 4: 29-31)***
- Lazima Musa alisisimka kuona Mungu akimtayarishia njia aliporudi Misri. Rejea wale ambao katika habari hii waliwezesha mpango wa Mungu kusonga mbele - Yethro, Haruni, viongozi, na watu. *Musa na Haruni walipaswa kuwasilisha mpango huo kwa nani wengine? Sisitiza kwamba ingawa haingekuwa rahisi, bado wangeweza kumtegemea Mungu ili kuwezesha mambo yafanyike. Mungu alikuwa ndiye mwezeshaji wa mambo yote!*

**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**

**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Musa aleta ujumbe wa Mungu.

**JIFUNZE**

Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Kutoka 4: 15b*** Hakikisha watoto wanaelewa muktadha wa mstari huu unaohusiana na Musa na Haruni walivyoshirikiana na wakati huohuo Mungu akiwa pamoja nao.

**KUMBUKA**

Rejea maisha ya Musa hadi wakati huu, kwa kutumia maswali kutoka kwenye habari zilizotangulia pamoja na hizi za Habari ya 4:
- Ni nani aliyerudi Misri pamoja na Musa?
- Ni nani alikutana naye njiani?
- Watu walijuaje kwamba Musa alikuwa ametumwa na Mungu?
- Eleza moja ya miujiza ambayo Musa alifanya mbele ya watu.

<u>**B10 Habari ya Kwanza**</u>

**Musa na pigo la kwanza – Habari hii inahusu kumtii Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Amri za Mungu zinahitaji kusikilizwa na kuzitii.<br>• Kukataa kusikiliza na kutomtii Mungu siku zote kutaishia kwenye adhabu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yeremia 38: 20***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Kutoka 7: 1-24*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza na watoto kuhusu sheria tunazopaswa kuzitii na matokeo ya kutotii, labda katika mazingira ya shule au katika jamii pana. Huenda ikafaa kurejea habari ya 4 ya B9 kwa maswali machache ili kuunganisha na maudhui ya leo. |
| **FUNDISHA** | • Sasa wakati ulikuwa umefika wa Musa na Haruni kumtaka Farao awaruhusu Waisraeli watoke Misri ili waweze kumwabudu Mungu jangwani. *Waulize watoto kubashiri majibu yake. Elezea kukataa kwake na matokeo ambayo yalifanya mambo kuwa mabaya zaidi kuliko hapo awali. Wasaidie watoto waone kwamba Farao hakumtii Mungu. Je, ungefikiria nini kuhusu Musa kama ungekuwa Mwisraeli?* ***(Kutoka 5: 1-21)***<br>• Musa hakuweza kuelewa kwa nini Mungu aliruhusu jambo hili litokee. Alimuuliza Mungu kuhusu hilo. Mungu aliwapa ahadi kwamba ataonyesha uweza wake mkuu na ingawa Farao mwanzoni hangetii, hatimaye Mungu angemfanya atende kile alichomtaka kufanya. *Wakumbushe watoto kwamba tunatoa ahadi na kuzisahau, au hatuwezi kuzitimiza, lakini ahadi za Mungu zitatimia daima.*<br>• Mungu alisema mrudie Farao tena na kumtaka awaachie watumwa Waisraeli! ***(Kutoka 5: 22-7: 5)***<br>• Wakati huu, Farao aliomba muujiza na fimbo ya Haruni ikawa nyoka. Waganga wa Farao walifanya vivyo hivyo, lakini nyoka wa Haruni alikula nyoka wote wa kichawi. *Hii ilionyesha nini kuhusu Mungu?* Bado Farao hangemtii Mungu. ***(Kutoka 7: 8-12)***<br>• Kisha Mungu akawaambia Musa na Haruni wakutane na Farao kando ya Mto Nile. Amri ya Mungu ilitolewa tena. Ikiwa Farao hangetii, Mto Nile ungegeuzwa kuwa damu, na hakungekuwa na maji safi na samaki wote wangekufa. Farao alikataa kusikiliza. Biblia inasema akageuka na kuingia nyumbani kwake. *Jadili mtazamo wa Farao - ni maneno gani yanauelezea? Eleza kwamba Biblia inamtaja kuwa na moyo mgumu.* ***(Kutoka 7: 14-23)***<br>• *Kwa hiyo, Wamisri wote wakachimba pande zote za mto kutafuta maji ya kunywa kwa sababu hawakuweza kunywa maji ya mto huo. Hili lilikuwa pigo la kwanza na lilidumu kwa siku 7.* ***(Kutoka 7: 24-25)***<br>• *Musa na Haruni walifanya kama vile Mungu alivyowaambia wafanye, wakitii kila jambo. Hivi ndivyo tunapaswa kujaribu na kufanya kila wakati. Biblia inasema kwamba Mungu anafurahia utii wetu! Farao hakumtii Mungu na alikataa kumsikiliza na kufanya hivyo siku zote huishia kwenye matatizo na adhabu ya Mungu. Jadili aina ya mambo ambayo Mungu anatuamuru tufanye katika maisha yetu ya kila siku.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Musa na pigo la kwanza. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu - ***Yeremia 38: 20*** ukisisitiza utiifu wa Musa na Haruni tofauti na kutotii kwa Farao, na changamoto kwamba tunapaswa pia kutii Neno la Mungu kila siku. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kukumbushia habari.<br>• Mungu alitoa ahadi gani kwa Musa na Haruni?<br>• Ni muujiza gani wa kwanza ambao Haruni alifanya?<br>• Ni nini kilitokea kwenye Mto Nile katika pigo la kwanza?<br>• Wamisri hawakuwa na nini kwa siku saba?<br>• Mungu anatuamuru tufanye mambo ya aina gani katika maisha yetu ya kila siku? |

<u>**B10 Habari ya Pili**</u>

**Musa na pigo la mwisho – Habari hii inahusu mpango wa Mungu kwa ajili ya kuwaokoa Waebrania.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Kukataa kumtii Mungu kwa Farao na Wamisri kulisababisha waadhibiwe.<br>• Mungu hawezi kupuuza dhambi, lakini hutoa njia ya wokovu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Kutoka 12: 13***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Kutoka 11: 1-10, 12: 1-13*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadili jinsi tunavyolindwa katika hali fulani. Chagua mifano ambayo watoto wanaweza kuhusianisha. K.m. kupaka krimu ya jua hulinda watu wenye ngozi nyeupe kutokana na hatari ya jua. Kubeba pasipoti ya kusafiria kunatuwezesha kupita kutoka nchi moja hadi nyingine bila kuogopa kukamatwa. Chanjo inatuzuia kupata ugonjwa. Katika habari ya leo, tutajifunza jinsi Mungu alivyowapa Waisraeli ishara maalum ili kuhakikisha kwamba wanakuwa salama wasipate adhabu Yake. |
| **FUNDISHA** | • Kulikuwa na mapigo tisa hadi sasa, lakini kila wakati Farao alikataa kuruhusu Waisraeli waondoke. Mungu alikuwa akiufanya moyo wa Farao kuwa mgumu mpaka Farao akatambua jinsi Mungu alivyo mkuu.<br>• Farao alikuwa amemwambia Musa kwamba hataki kumuona tena. ***(Kutoka 10: 27-29)*** Lakini Mungu alikuwa amemweleza Musa pigo la mwisho lingekuwa nini. Kungekuwa na adhabu ya kutisha kwa kila familia, kila mwana mkubwa kuliko wote katika kila familia alikuwa anaenda kufa. ***(Kutoka 11: 4-6)*** *Lakini Farao hakuamini kwamba Mungu angeweza au angeleta adhabu hiyo ya kutisha.* ***(Kutoka 11: 10)***<br>• *Tunapaswa kujifunza kwamba chochote anachosema Mungu au kinachosemwa katika Biblia ni ukweli, na chochote Anachoahidi atakitimiza.*<br>• Mungu alimweleza Musa matayarisho ambayo Waisraeli walipaswa kufanya ili kujitayarisha kuondoka Misri. Kila familia ililazimika kuua mwana-kondoo. Kiasi cha damu kilipakwa kwenye miimo ya milango ya nyumba zao ambacho kingeonyesha kwamba nyumba hiyo ilikuwa ya Waisraeli. Kisha walipaswa kula mlo wa pekee wa mwana-kondoo aliyechomwa, mkate, na mboga chungu. Walitakiwa kula chakula haraka na kuvaa tayari kwa kuondoka haraka sana. Mungu alieleza kwamba Waisraeli watakuwa salama kama watakuwa na damu kwenye milango yao. ***(Kutoka 12: 12-13)***<br>• *Eleza kuhusu msisimko na matarajio ya ukweli kwamba hatimaye walikuwa karibu kuondoka na jinsi Waisraeli walivyofuata maelekezo kwa usahihi. Jadili thamani na umuhimu wa damu kwa Waisraeli na jinsi ilivyokuwa ulinzi wao pekee.*<br>• *Si rahisi kila mara kwetu kuelewa namna Mungu anavyofanya kazi, lakini tunaweza kuwa na uhakika kwamba Yeye ndiye anayejua kilicho bora zaidi kila wakati. Waisraeli waliwezaje kuwa salama? Vivyo hivyo, yeyote anayeamini kwamba Bwana Yesu alikufa msalabani anaokolewa kutokana na adhabu tunayokabiliana nayo kwa sababu ya dhambi zetu. Biblia inaeleza kwamba Bwana Yesu ni Mwana-Kondoo wa Mungu, si kwa Waisraeli tu, bali kwa ulimwengu wote, ikiwa ni pamoja na sisi. Tunapoitumainia damu yake iliyomwagika alipokufa msalabani, ndipo tutaokolewa na adhabu ya dhambi zetu.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Musa na pigo la mwisho. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu - ***Kutoka 12: 13*** |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kukumbushia habari.<br>• Ni neno gani jingine ambalo linaweza kutumika kwa ajili ya adhabu ya Mungu?<br>• Adhabu ya mwisho itakuwa ipi kwa Farao?<br>• Waisraeli walipaswa kufanya nini ili kuhakikisha kwamba wanakuwa salama?<br>• Walipaswa kula nini? Jinsi gani walilazimika kula?<br>• Bwana Yesu amefanyaje iwezekane kwetu kuokolewa? ***(Warumi 5: 8)*** |

**B10 Habari ya Tatu**

**Musa na kutoka Misri – Habari hii inahusu uwezo wa ajabu wa Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu aliwaokoa Waisraeli kama alivyoahidi alipozungumza na Musa kwenye kijiti kilichowaka moto.<br>• Mara nyingi Biblia hurejelea tukio hili kuwa mojawapo ya mifano mikuu ya nguvu za Mungu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Kutoka 14: 30a***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Kutoka 12: 31-39, 14: 1-31*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Taja baadhi ya mambo ambayo haiwezekani sisi kufanya. K.m. Kuruka bila ndege, kuvuka bahari bila mashua, kutafuta njia kupitia jangwani bila dira n.k. Hata hivyo, lisilowezekana kwa wanadamu linawezekana kwa Mungu. Alikuwa anaenda kuonyesha mojawapo ya udhihirisho mkuu wa nguvu zake katika Biblia. |
| **FUNDISHA** | • Usiku, wakati wazaliwa wote wa kwanza wa Misri walipokufa, Farao akatuma watu kuwaita Musa na Haruni. *Mwitikio wa Farao ulikuwaje baada ya mapigo yote yaliyotangulia? Eleza jinsi wakati huu ulivyokuwa tofauti* - Aliwaambia wachukue watu wote, na mifugo yao na kuondoka Misri mara moja. ***(Kutoka 12: 31-32)*** Wamisri pia waliwahimiza waondoke kwa sababu waliogopa kwamba wangekufa wote kama Waisraeli wangebaki.<br>• Hata waliwapa zawadi za fedha, dhahabu, na nguo walipoondoka. ***(Kutoka 12: 35-36)*** Kwa jumla, kulikuwa na wanaume zaidi ya mia sita elfu na pia wanawake na watoto. *Kwa kushirikiana na watoto wakubwa unaweza kujaribu kulinganisha namba hii na idadi ya watu mahali fulani wanapopajua.*<br>• Mwishoni Farao alikuwa akimtii Mungu! Angeweza kuepuka kuteseka sana kama angefanya hivyo mwanzoni. *Kwa mara nyingine tena, sisitiza umuhimu wa utii kwa wazazi, walimu, na muhimu zaidi, kwa Mungu!*<br>• Waisraeli wakiongozwa na Musa walisafiri kuelekea Bahari ya Shamu. *Chunguza hisia zao.* Lakini haikuwa mara ya mwisho kumuona Farao! Tena, Mungu aliufanya moyo wa Farao kuwa mgumu, kwani bado alipaswa kujifunza jinsi Mungu alivyo mkuu! Ghafla Farao akagundua kuwa amepoteza wajenzi wake wote na akaamua kuwakimbiza kwa magari 600. ***(Kutoka 14: 3-7)***<br>• Waisraeli walinaswa! Farao alikuwa nyuma yao na Bahari ya Shamu ilikuwa mbele yao. Unafikiri walijisikiaje sasa? Eleza hofu yao na jinsi walivyomlaumu Musa. Lakini Musa aliwaambia wasimame imara na wataona ukombozi ambao Mungu atawaletea! ***(Kutoka 14: 10-14)***<br>• Bwana alimwambia Musa ainue fimbo yake juu ya bahari. Musa alipotii, njia kavu ilitokea kimuujiza katikati ya Bahari ya Shamu ili Waisraeli wote waweze kupita kwenye nchi kavu.<br>• *Eleza kilichotokea Wamisri walipojaribu kuwafuata.* Musa aliinua fimbo yake tena na maji yakarudi. Biblia inasema kwamba jeshi lote la Farao lilifunikwa na maji na hakuna hata mmoja wao aliyeokoka. ***(Kutoka 14: 28)*** *Ungewaza nini kuhusu Mungu kama ungekuwa Mwisraeli? Eleza majibu yao kuhusu uwezo mkuu wa Mungu - walimcha Bwana (eleza) na kuweka imani yao Kwake na kwa Musa.* ***(Kutoka 14: 31)***<br>• Sisi pia tunaweza kumwamini Bwana daima kwa sababu ya uweza Wake mkuu. Kama walivyofanya Waisraeli, ni lazima tumwamini Yeye na kisha tunaweza kusema, "Bwana aliniokoa MIMI!"<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Musa na kutoka Misri. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu - ***Kutoka 14: 30a*** |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kukumbushia habari.<br>• Kwa nini Farao aliamua kuwaruhusu Waisraeli waende zao?<br>• Wamisri waliwapa nini?<br>• Kwa nini Farao aliamua kuwafukuza?<br>• Farao alitumia magari mangapi ya vita?<br>• Kwa nini Waisraeli waliingiwa na hofu?<br>• Mungu alimwambia Musa afanye nini ambacho kingewaokoa?<br>• Ni nini kilitokea kwa jeshi la Misri?<br>• Waisraeli walifanya nini walipoona jambo lililotukia? |

**<u>B10 Habari ya Nne</u>**
**Musa na Israeli wamshukuru Mungu – Habari hii inahusu kumsifu Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Waisraeli walishukuru kwa yote ambayo Mungu alikuwa amefanya ili kuwapa uhuru na usalama.<br>• Sote tunapaswa kusimama, kutazama nyuma na kumshukuru Mungu kwa yale ambayo ametufanyia katika maisha yetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Zaburi 106: 1***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Kutoka 15: 1-22*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Tumia vidokezo kukumbuka baadhi ya mambo ya ajabu ambayo yameandikwa katika Biblia. K.m. Danieli aliokoka katika tundu la simba, Daudi akamuua Goliathi nk, ikiwa ni pamoja na kuvuka Bahari ya Shamu kama katika habari ya wiki iliyopita. Tafuta matukio kwenye Biblia ikiwa unayo. Eleza kwamba katika kila moja ya haya, wahusika wa Biblia hawakuwa na njia nyingine ila kutegemea nguvu kuu za Mungu. Tutajua jinsi Waisraeli walivyofanya baada ya Mungu kuwaokoa na kufikiria jinsi tunavyopaswa kumjibu Mungu kwa yale ambayo ametufanyia. |
| **FUNDISHA** | • Hatimaye Waisraeli walikuwa huru kutoka kwenye utumwa na adui zao wote walikuwa wamezama baharini. *Eleza jinsi walivyohisi.* Walijua ni Mungu ndiye aliyekuwa amewaokoa, na walishukuru sana kiasi kwamba walitaka kumsifu Mungu kwa yale ambayo amefanya. ***(Kutoka 15: 1)*** Walitambua jinsi Mungu alivyokuwa mkuu na wakaimba juu ya Ukuu wake kwa sababu walijua kwamba hakuna Mungu mwingine aliyekuwa na nguvu hizo. ***(Kutoka 15: 11)*** Waliimba kwa uzito kuhusu yote ambayo alikuwa amewafanyia.<br>• *Watoto wanapaswa kutambua jinsi Mungu alivyo mkuu: 1) Katika Uumbaji. 2) Katika kutimiza mahitaji yetu yote kila siku. 3) Kwa upendo Wake mkuu katika kumtuma Mwanawe kufa msalabani kwa ajili yetu.*<br>• Waisraeli hawakuimba tu kuhusu Mungu, walikuwa na uhusiano wa karibu naye, kwa hiyo walimwita "Mungu wangu", "Nguvu zangu", "Wokovu wangu". ***(Kutoka 15: 2)***<br>• *Watoto wanaweza kupewa changamoto iwapo wanajua tu kuhusu Mungu, au kama wana uhusiano wa kibinafsi Naye na wanamjua Yeye kama Baba yao wa Mbinguni.*<br>• Waisraeli hawakufikiria tu kuhusu wakati uliopo, walijua kwamba wangeweza kumwamini Yeye kwa ajili ya vita vya baadaye na maadui wengine walipokuwa wakielekea kwenye Nchi ya Ahadi. *Tunaweza kujifunza kwamba Bwana habadiliki kamwe, na tunaweza kumwamini si leo tu, bali daima katika siku zijazo.*<br>• Miriamu, dada yake Haruni, aliongoza baadhi ya wanawake katika kuimba na kucheza. Walifurahi sana waliposherehekea yale ambayo Mungu alikuwa amefanya.<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Musa na Israeli wamshukuru Mungu / Musa amshukuru Mungu. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu - ***Zaburi 106: 1*** - Mstari huu unatukumbusha kuhusu kumshukuru Bwana ili watoto waweze kutiwa moyo kufanya baadhi ya maombi ya shukrani kwa yale ambayo Bwana amewatendea. |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kurejelea habari au maswali yote ya B10.<br>• Waisraeli walifanya nini walipoona wako huru?<br>• Je, walimwelezeaje Mungu katika wimbo wao?<br>• Waisraeli walijua nini kuhusu wakati ujao?<br>• Nani aliongoza wanawake katika kuimba na kucheza?<br>• Unafikiri ni kwa nini Waisraeli walibadilika kutoka kuwa wenye hofu na woga hadi kuimba na kumsifu Mungu? |

## B11 Habari ya Kwanza

**Mungu atoa chakula – Habari hii inahusu Mungu kutoa chakula kwa ajili ya Waisraeli.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu aliwapa Waisraeli chakula kwa miaka arobaini jangwani.<br>• Bwana Yesu ndiye "Mkate wa Uzima" na anakidhi mahitaji yetu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 6: 35***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Kutoka 16: 1-32*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Wakumbushe watoto kwa ufupi kuhusu kile kilichotokea katika B9 na B10. Mungu alikuwa amewaonesha Waisraeli uwezo wake katika kuwaokoa kutoka Misri na sasa aliahidi kuwaongoza hadi nchi mpya. Hawakukawia njiani hadi watu walipoanza kunung'unika na kulalamika kwa Musa kuhusu njaa! Chakula chao kilikuwa kimekwisha, nao walikuwa wakiwaza kurudi Misri na kukumbuka chakula chote walichokifurahia huko. ***(Kutoka 16: 2-3)*** Tayari walikuwa wamesahau kwamba Mungu alikuwa na sababu na kwamba alijua mahitaji yao yote kwa ajili ya safari yao.<br>*Ikiwezekana, unaweza kuwakumbusha watoto kwamba huu ni mtazamo mbaya. Mungu anataka tuwe na shukrani kwake.* |
| **FUNDISHA** | • Ingawa watu walishindwa kumwamini Mungu, alionesha kwamba bado anawajali. Mungu alikuwa na mpango wa kuhakikisha kwamba watakuwa na chakula daima. Alituma mkate kutoka Mbinguni na walipaswa kuukusanya kila asubuhi. Siku ya sita ya juma walipaswa kukusanya mara mbili zaidi ili chakula kiwepo hadi Siku ya Sabato (siku maalum ya Mungu). Kila jioni walipokea nyama. ***(Kutoka 16: 4-12)***<br>• *Waza kuhusu Waisraeli wakitoka kwenye hema zao asubuhi na kueleza jinsi walivyoitikia kwa kile walichokipata.* Musa alieleza kwamba huu ndio mkate ambao Bwana alikuwa amewapa. Kila mtu alipaswa kukusanya kiasi cha kutosha kwa ajili ya watu wanaoishi katika hema yao. Hakuna mtu aliyepaswa kuweka chochote kwa ajili ya siku iliyofuata. Watu wengine, hata hivyo, walijaribu kuhifadhi lakini siku iliyofuata mkate ulikuwa imeharibika. ***(Kutoka 16: 15-20)*** *Onesha umuhimu wa kufanya kama vile Mungu asemavyo, badala ya kufanya kama uonavyo mwenyewe.*<br>• Watu waliuita mkate kutoka Mbinguni "Mana". Ulikuwa na ladha kama asali! Mungu alituma mana kwa Waisraeli kwa muda wote wa safari yao. Mungu alikuwa amewapa uthibitisho zaidi kwamba ni Mungu wao na angewatunza. ***(Kutoka 16: 31-32)***<br>• Katika habari yetu, Waisraeli walipaswa kukusanya na kula mana kabla ya kutosheleza njaa yao. Mana iliwapa nguvu kila siku jangwani, lakini sikuzote walihitaji mana zaidi.<br>• *Miaka mingi baadaye, Yesu alishuka kutoka Mbinguni kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Alijiita "Mkate wa Uzima". Tukimpokea Bwana Yesu, (Mkate wa Uzima) maishani mwetu, Yeye hutupatia uzima wa milele – uzima ambao tunaufurahia hapa na Mbinguni. Mana kutoka Mbinguni ilikuwa muujiza wa ajabu kwa Waisraeli lakini kwa kumpokea Bwana Yesu tunaweza kuwa na kitu kikubwa zaidi. (Unaweza kufanya fundisho hili lieleweke zaidi kwa kuweka habari kuhusu mana na Mkate wa Uzima katika safu mbili kwenye ubao au chati.)*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mungu atoa chakula / Mungu awapa Waisraeli chakula. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Yohana 6: 35***. Kazia yaliyosemwa hapo juu. |
| **KUMBUKA** | Tumia maswali haya katika zoezi.<br>• Kwa nini watu walinung'unika?<br>• Walilalamika kwa nani?<br>• Je, walipaswa kufanya nini badala ya kulalamika?<br>• Ni siku ngapi kila juma mana ilionekana ardhini?<br>• Walipata nini kila jioni?<br>• Walikusanya mana kwa muda gani?<br>• Yesu alitumia jina gani kwa ajili Yake Mwenyewe?<br>• Yesu ni mkuu kuliko mana kwa njia gani? |

## B11 Habari ya Pili

**Mungu atoa ushindi – Habari hii inahusu Mungu kuwasaidia wanaomtumaini.**

**Tunajifunza kuwa:**
- Mungu aliwasaidia Waisraeli walipomtegemea.
- Mungu anatutaka tumuombe ili tuwe na ushindi katika maisha yetu.

**Mstari Muhimu:** ***Kutoka 17: 15***
**Habari kwenye Biblia:** ***Kutoka 17: 8-15***

### TOA UTANGULIZI

Punde Waisraeli walikabiliana na tatizo jingine. Jeshi la adui lililoitwa Waamaleki lilianza kuwashambulia. ***(Kutoka 17: 8)***
*Tumia maswali hapo chini kuwasaidia watoto katika kufikiri kuhusu hali hiyo:*
- *Waisraeli walipaswa kufanya nini? (kupigana)*
- *Je, walizoea kupigana? Wakumbushe watoto kwamba huko Misri walikuwa watumwa, sio askari.*
- *Walijisikiaje?*
- *Je, waliweza kutegemea msaada wa Mungu? Wakumbushe watoto kwamba Mungu alikuwa amewatoa Misri ili kuwaleta katika nchi mpya. Angetimiza ahadi yake.*

### FUNDISHA

- Musa alikuwa kiongozi mwenye hekima na alijua la kufanya. Alimwomba msaidizi wake Yoshua achague jeshi. Musa alijua kwamba jeshi lingehitaji msaada wa Mungu, kwa hiyo akaenda pamoja na Haruni na Huri kwenye kilele cha kilima kinachotazama uwanja wa vita. Musa aliinua fimbo yake (fimbo ndefu ambayo aliitumia alipokuwa mchungaji) juu ya kichwa chake kwa kutumia mikono miwili. Eleza kwamba hii ilikuwa njia ya kuonyesha kwamba Waisraeli walikuwa wakimtumaini Mungu ili kuwasaidia kushinda. ***(Kutoka 17: 9)***
- Muda wote Musa alipofanya hivyo, Waisraeli walikuwa wakishinda. *Waambie watoto washike mikono yao juu ya vichwa vyao. Unafikiri nini kingetokea kwenye mikono yako ikiwa utaiweka juu namna hiyo kwa muda mrefu?* Punde mikono ya Musa ilichoka na akaishusha chini kwa ajili ya kupumzika. Kisha adui akaanza kushinda. *Waombe watoto wapendekeze jinsi Haruni na Huri wangeweza kumsaidia Musa na kisha kufafanua kile walichofanya.* Kisha Musa aliweza kuinua mikono yake hadi jua lilipotua na kufikia wakati huo Waisraeli walikuwa wameshinda. Musa alitaka kumshukuru Mungu kwa ushindi huo, kwa hiyo akajenga madhabahu ya mawe na kuiita “Bwana ni Bendera yangu.” *Eleza kwamba Musa alitaka Mungu apate heshima yote kwa ushindi huo.* ***(Kutoka 17: 10-13, 15)***
- *Je, unadhani nani alikuwa na sehemu muhimu katika kushinda vita? Yoshua na askari hawangeweza kushinda vita hivi kama Musa hangeinua mikono yake kwa Mungu na kumtegemea. Ikiwa tumemwamini Bwana Yesu kama Mwokozi wetu, tuna adui pia - Shetani. Anataka kutufanya tuogope na kutuondolea furaha maishani mwetu. Ni nani aliye na nguvu zaidi Bwana Yesu au Shetani? Kwa sababu Yesu ana nguvu zaidi, tunaweza kupata ushindi. Tunahitaji kumtegemea Yeye kila wakati.*

**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**

**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mungu atoa ushindi.

### JIFUNZE

Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Kutoka 17: 15.***

### KUMBUKA

Watoto wanaweza kutengeneza bendera kubwa iliyopambwa ikisema, “Bwana ni Bendera yangu.” Vinginevyo, maswali haya yanaweza kutumika katika zoezi:
- Ni nani alikuwa kiongozi wa jeshi la Israeli?
- Musa alienda wapi?
- Nani walienda na Musa?
- Nini kilitokea kwenye vita wakati Musa alipoinua mikono yake?
- Musa aliinua mikono yake kwa muda gani?
- Nani alitoa ushindi?
- Nani ni adui yetu?
- Tunahitaji kumtegemea nani atusaidie?

**<u>B11 Habari ya Tatu</u>**

**Mungu atoa amri – Habari hii inahusu sheria za Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu ni mtakatifu.<br>• Hatuwezi kushika amri za Mungu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Kutoka 20: 1 au Warumi 3: 23***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Kutoka 19-20*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu sheria ulizo nazo shuleni au nyumbani. Ni zipi? Kwa nini tuna sheria? Je! ni rahisi kila wakati kushika sheria?<br>Katika somo la leo tutajifunza jinsi Mungu alivyotoa sheria zake kwa Waisraeli. |
| **FUNDISHA** | • Waisraeli walifika kwenye mlima mkubwa uitwao Sinai ambapo walipiga kambi. Mungu alimweleza Musa kwamba angeshuka katika wingu zito hadi juu ya mlima. Musa alipaswa kuweka mawe ya alama kuzunguka sehemu ya chini ya mlima ili watu wasijaribu kupanda juu. Ingawa watu walikuwa walijiosha na kujitayarisha, dhambi yao ilimaanisha kwamba hawakuweza kumkaribia Mungu. ***(Kutoka 19: 1-14)***<br>• Siku tatu baadaye watu walisimama chini ya mlima. Moshi ulitoka mlimani na mlima ukatikisika. *Eleza kwamba hii ilionyesha watu jinsi Mungu alivyokuwa na nguvu. Tafakari jinsi watu walivyojisikia.* Kisha Mungu akamwita Musa apande juu na kwa mara ya pili, akamwambia Musa awaonye watu wasimame chini ya mlima. ***(Kutoka 19: 16-22)*** *Eleza kwamba watu hawakuweza kumkaribia Mungu kwa sababu Yeye ni Mtakatifu (asiye na dhambi yoyote) lakini walikuwa na dhambi maishani mwao. Leo, bado dhambi inatutenganisha na Mungu isipokuwa pale tu dhambi zetu zinaposamehewa.*<br>• Baadaye, Musa alipokea amri kumi kutoka kwa Mungu, zilizoandikwa juu ya mawe mawili makubwa. Amri zilikuwa kanuni au sheria za Mungu na ziliweka wazi kwa watu jinsi Mungu alivyotarajia watende. Walipaswa kumpenda Mungu kuliko mtu mwingine yeyote na pia walipaswa kupendana wao kwa wao. *Kwa watoto wa Daraja la 2 ingefaa kuzisoma na kueleza kila moja kwa ufupi, ikionyesha kwamba amri 1-4 zinahusu jinsi tunavyomtendea Mungu, na amri 5-10 jinsi tunavyowatendea wengine. Wasaidie waelewe kwamba tumeshindwa kuzitii!* ***(Kutoka 20: 1-17)***<br>• *Inasikitisha kwamba Waisraeli hawakuweza kushika sheria za Mungu, na sisi pia hatuwezi. Sisi sote tunapungukiwa na kile ambacho Mungu anatazamia. Sisi ni wenye dhambi. Bwana Yesu ndiye mtu pekee aliyeishi maisha makamilifu duniani. Hii ndiyo sababu ana uwezo wa kuwa Mwokozi wetu. Alikufa ili kuchukua adhabu ya dhambi zetu ili Mungu atusamehe. Kisha tunaweza kuwa katika familia ya Mungu na bila kulazimika kukaa mbali Naye kama Waisraeli walivyofanya.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mungu atoa amri. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Kutoka 20: 1 au Warumi 3: 23.*** |
| **KUMBUKA** | Kwa ajili ya zoezi unaweza kuzingatia amri zenyewe kama zilivyoandikwa katika somo la Daraja la 2. Ikiwezekana, ziandikwe ubaoni/chati ili watoto waweze kuziona na kuzisikia. Baada ya kuzisoma zote, ondoa orodha. Acha neno muhimu katika kila amri. k.m. Usiwe na ______ mingine ila mimi. Usijifanyie ________. Ikiwa mtoto anajua neno linalokosekana, anaweza kupata alama kwa ajili ya timu yake.<br>Watoto wadogo wangeweza kusaidia kutengeneza kielelezo cha Mlima Sinai. Tengeneza umbo la koni kwa kadi, bandika pamba juu kwa ajili ya wingu, tengeneza miale myekundu ya moto na vipande vya utepe uliojizungusha kuwakilisha mawingu ya radi na mwanga. Weka uzio kuzunguka chini. Watoto wanaweza kuongeza hema ndogo. |

**B11 Habari ya Nne**

**Mungu atoa wokovu – Habari hii inahusu njia ya Mungu ya kuwaokoa watu na mauti.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alitoa njia kwa ajili ya Waisraeli kuepuka adhabu waliyostahili.<br>• Mungu ametoa njia kwa ajili yetu kuokolewa.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 3: 14***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Hesabu 21: 4-9*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Wakati mwingine tunarudia kosa lile lile! Je, unaweza kukumbuka Waisraeli walifanya nini wakati chakula walichokileta kutoka Misri kilipoisha? Ndiyo, walinung'unika na kulalamika! Na katika habari ya leo wananung'unika tena! Hebu tujue ni kwa nini.<br>Au<br>Ongea juu ya hatari ya kuumwa na nyoka, hitaji la kwenda hospitalini na kupata dawa ya kuzuia madhara ya sumu. Katika habari ya leo Mungu alikuwa na tiba tofauti sana kwa wale waliokuwa wameumwa na nyoka. |
| **FUNDISHA** | • La kusikitisha, Waisraeli walimsema vibaya Musa na Mungu, wakisema kwamba mambo yalikuwa mazuri huko Misri na kwamba walichukia mana ambayo Mungu aliwapa. Kiasi gani walikosa shukrani! ***(Hesabu 21: 5)***<br>• Wakati huu Mungu alikasirishwa na watu na akaamua kuwaadhibu. Mara kambi hiyo ilivamiwa na nyoka wenye sumu. *Nini kingetokea kwa watu?* Ndiyo, watu waliumwa na wengi wao walikufa. Moja kwa moja watu wakajua ni makosa yao. Walienda kwa Musa na kusema kwamba walikuwa wametenda dhambi na kumwomba aombe Mungu awaondoe nyoka hao. ***(Hesabu 21: 6-7)*** *Wasaidie watoto watambue kwamba huo ndio mtazamo unaofaa tunapofanya makosa. Tunahitaji kukiri dhambi zetu na kumwomba Mungu atusaidie.*<br>• Baada ya Musa kumwomba Mungu, Mungu alimwambia Musa afanye jambo la ajabu. Ilimbidi atengeneze nyoka wa shaba na kumweka juu ya nguzo kambini. Nyoka wa shaba anayeng'aa alikuwa ndani ya upeo wa macho ya kila mtu. Mungu aliahidi kwamba yeyote aliyeumwa hatakufa kama angemtazama nyoka kwenye mti. Kila mtu aliyeamini hivyo na kufanya kama Mungu alivyosema, aliishi. Ni njia rahisi kama nini ya kuepuka kifo! ***(Hesabu 21: 8-9)*** *(Ikiwa ulitumia wazo la pili katika utangulizi, unaweza kufanya ulinganisho.) Je, unafikiri Waisraeli walitii maagizo ya Mungu? Kwa nini? Sisitiza kwamba hii ndiyo ilikuwa njia pekee kwa ajili yao kuishi - haingesaidia kujaribu kitu kingine chochote!*<br>• Miaka mingi baadaye, Yesu alipokuwa duniani, alitumia habari hii kufundisha kila mtu somo muhimu. Sisi ni kama Waisraeli kwa sababu tumemtenda Mungu dhambi na dhambi zetu zitaadhibiwa. Lakini Mungu ametuandalia njia ya kuepuka adhabu ya dhambi zetu. Yesu alieleza kwamba Yeye pia ‘angeinuliwa’ alipokufa kwa ajili ya dhambi zetu. Tunapoweka tumaini letu katika yale ambayo Yesu ametufanyia, Mungu hutuokoa na kutupa uzima wa milele. *Sisitiza kwamba ni kupitia Yesu pekee tunaweza kuokolewa na uwape watoto changamoto kuhusu hitaji lao la kuitikia.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mungu atoa wokovu. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Yohana 3: 14***. Taja kwamba haya ni maneno ya Yesu. Alieleza jinsi atakavyoweza kutuokoa wakati atakapoinuliwa juu ya msalaba. |
| **KUMBUKA** | Kikundi kidogo cha watoto kinaweza kutengeneza picha ya nyoka wa shaba kwenye nguzo na kikundi kingine kinaweza kutengeneza msalaba. Mstari Muhimu pia unaweza kuoneshwa kwenye mchoro uliokamilika.<br>Au watoto wanaweza kutengeneza nyoka kutokana na plastiki au udongo na kuwafunga kwenye penseli zinazowakilisha nguzo.<br>Au unaweza kuwa na zoezi kutokana na habari zote katika B11.<br>Maswali ya ziada katika B11 yanaweza kujumuisha:<br>• Wakati huu Waisraeli walinung’unikia nini?<br>• Mungu aliwaadhibuje?<br>• Watu walipaswa kufanya nini ili waponywe kutokana na kuumwa na nyoka?<br>• Tunawezaje kuokolewa kutoka kwenye adhabu ya dhambi zetu? |

# B12 Habari ya Kwanza

**Yusufu na malaika – Habari hii inahusu Yusufu kumtii Mungu, hata ilipokuwa vigumu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Jina la 'Yesu' lina maana ya 'Mwokozi'.<br>• Kama alivyofanya Yusufu, tunapaswa wakati wote kumsikiliza na kumtii Mungu.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 1: 21***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mathayo 1: 18-25*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuhusu majina na umuhimu wake - Waulize watoto kama wanajua maana ya majina yao au kwa nini walipewa majina yao.<br><br>Eleza kwamba leo watoto watakuwa wakijifunza kuhusu mtoto wa pekee sana katika Biblia ambaye alipewa jina la pekee sana. Ruhusu watoto kukisia habari itamhusu nani. |
| **FUNDISHA** | • Yusufu na Mariamu walikuwa wakipanga kuoana, lakini siku moja Mariamu alimwambia Yusufu kwamba alikuwa anatarajia mtoto. Yusufu alijua yeye si baba wa mtoto, hivyo akaamua kutomuoa Mariamu. ***(Mathayo 1: 18-19)***<br>• Usiku mmoja Yusufu aliota ndoto. Malaika alimtokea katika ndoto na kusema na Yusufu. Malaika akasema, "Usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu." ***(Mathayo 1: 20)*** *Waelezee watoto kwamba hilo linamaanisha kwamba mtoto huyo angekuwa Mwana wa Mungu.*<br>• Malaika alimwambia Yusufu kwamba anapaswa kumwita mtoto 'Yesu' kwa sababu atawaokoa watu kutoka katika dhambi zao. ***(Mathayo 1: 21)*** *Eleza kwamba maana ya Yesu ni "Mwokozi". Jadili mwokozi ina maana gani. (katika maisha ya kila siku, k.m. mtu aliye katika hatari ya kuzama anahitaji mwokozi au mwokoaji) Wape watoto maelezo ya kazi ya Yesu kama Mwokozi. Biblia inasema kila mtu anahitaji kuokolewa na adhabu ya dhambi - Yesu hakutenda dhambi hivyo aliweza kuchukua adhabu ya dhambi ya ulimwengu wote alipokufa msalabani. Biblia inasema kwamba kila mtu anahitaji kujuta kwa dhati kwa ajili ya dhambi yake, na kuwa tayari kumpokea Yesu kama Mwokozi.*<br>• Yusufu alipozinduka kutoka katika ndoto yake, alifanya kama alivyoambiwa hivyo akamuoa Mariamu. Muda fulani baadaye mtoto alizaliwa, na Yusufu akamwita 'Yesu'. ***(Mathayo 1: 24-25)*** *Waulize watoto kuhusu maagizo ambayo Yusufu alikuwa amepewa na mzungumzie jinsi alivyoyafuata. Eleza jinsi ilivyo muhimu sisi kusikiliza maagizo ya Mungu katika Biblia na kuyafuata. Kwa pamoja, fikiria na utengeneze orodha ya baadhi ya maagizo ambayo Mungu ametoa ili tuyafuate.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Yusufu na malaika. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Mathayo 1: 21.*** |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kukumbushia habari.<br>• Yusufu alitaka kumuoa nani?<br>• Habari gani Mariamu alimwambia Yusufu?<br>• Mungu aliongeaje na Yusufu?<br>• Baba wa mtoto alikuwa nani?<br>• Ilikuwa mtoto aitwe nani?<br>• Maana ya jina 'Yesu' ni nini?<br>• Yusufu alifanya nini baada ya kuamka kwenye ndoto?<br>• Tunahitaji kuokolewa kutokana na nini? |

**<u>B12 Habari ya Pili</u>**

**Mamajusi na Herode – Habari hii inahusu Mamajusi kujaribu kumtafuta Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu ni Mfalme wa wafalme.<br>• Yesu anastahili kuabudiwa.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 2: 2***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mathayo 2: 1-8*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize watoto kufikiria kuhusu watu muhimu. Tengeneza orodha yao au uwe na baadhi ya picha zao.<br>Jadili – Je, ungependa kukutana na yeyote kati ya watu hao? Ungekutana na mmojawapo ungesemaje? Ungefanya nini? Ungewatendea nini?<br>Waambie watoto kwamba leo tutajifunza kuhusu watu fulani ambao walisafiri kutafuta mtu muhimu zaidi aliyepata kuishi. |
| **FUNDISHA** | • Siku moja baadhi ya Mamajusi walioishi mbali na mahali Yesu alipozaliwa, waliona nyota mpya angani. *Onesha msisimko wao walipotambua maana ya nyota hiyo. Eleza jinsi walivyosafiri kutoka Mashariki kwa safari ndefu (miezi!) na hatimaye kufika kwenye Kasri ya Mfalme Herode.* Simulia walichomwambia Mfalme Herode “Yuko wapi yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Tuliiona nyota yake ilipotokea angani na tumekuja kumsujudia”. ***(Mathayo 2: 1-2)*** *Waelezee watoto hao kwamba Mfalme mpya ambaye angezaliwa ni Yesu, Mwana wa Mungu na kwamba angekuwa mkuu kuliko Mfalme mwingine yeyote aliyepata kuishi. Yesu ni Mfalme wa Wafalme. Waulize watoto kama wanaweza kukumbuka jina la Yesu linamaanisha nini kutoka kwenye somo lililopita. Jadili Mamajusi walimaanisha nini waliposema wanataka ‘kumsujudia’ Mfalme? Kwa nini Yesu alistahili kusujudiwa?*<br>• Herode aliposikia kuhusu Mfalme mpya, alikuwa na wasiwasi. Hakutaka mtu mwingine yeyote achukue nafasi yake kama Mfalme. Aliwaita baadhi ya washauri wake na kuwauliza ni wapi Mfalme mpya alipaswa kuzaliwa. Walichunguza Maandiko na kugundua kwamba mtoto huyo angezaliwa katika mji unaoitwa Bethlehemu. ***(Mathayo 2: 3-6)***<br>• Herode akawaita wale Mamajusi akawaambia, “Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto; na mkiisha kumwona, nileteeni habari, ili mimi nami niende nimsujudie.” ***(Mathayo 2: 7-8)*** *Eleza kwamba Herode hakutaka kabisa kumsujudia Mfalme huyo mpya; alichotaka hasa ni kumuua. Waulize watoto kwa nini wanafikiri Herode alitaka kumuua Mfalme mpya. Eleza kwamba watu wengi leo bado hawamtendei Yesu jinsi wanavyopaswa, lakini Mungu anataka tumpende na kumwabudu Yesu kama wale Mamajusi walivyomtendea.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mamajusi na Herode. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, inapobidi, Mstari Muhimu. ***Mathayo 2: 2.*** |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kukumbushia habari.<br>• Nini kilitokea angani?<br>• Mamajusi walitoka upande gani?<br>• Walikwenda wapi, kumtafuta Mfalme mpya?<br>• Aliitwa jina gani Mfalme waliyeongea naye?<br>• Mfalme Herode alijisikiaje aliposikia kuhusu Mfalme mpya?<br>• Mji gani waligundua kwamba Mfalme alipaswa kuzaliwa huko?<br>• Herode aliwaambia Mamajusi wafanye nini?<br>• Nani ni mkuu kuliko Mfalme mwingine yeyote? |

**B12 Habari ya Tatu**
**Mamajusi na Yesu – Habari hii inahusu Mamajusi kuifuata nyota na kumpata Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mamajusi walimuabudu Yesu na kumpa zawadi za kipekee sana.<br>• Tunaweza bado kumuabudu Yesu leo.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 2: 11***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mathayo 2: 9-12*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadili – Ni zawadi gani bora zaidi ambayo umewahi kupewa? (Unaweza kuwaambia watoto wachore picha yake). Ikiwa ungemtembelea mtoto ambaye ndio kazaliwa ungempa zawadi gani?<br><br>Waelezee watoto kwamba leo tutakuwa tunajifunza kuhusu zawadi ambazo Mamajusi walitoa. Waulize watoto wakuambie kile walichojifunza kuhusu Mamajusi katika somo lililopita. |
| **FUNDISHA** | • Mamajusi wakamwacha Herode wakaenda zao. Waliiona tena ile nyota na ikawaongoza mpaka mahali ambapo Yesu alikuwa. ***(Mathayo 2: 9-10)*** *Jadili jinsi Mamajusi walivyohisi walipoiona nyota. Kwa nini walihisi hivyo?*<br>• Mamajusi walifika kwenye nyumba huko Bethlehemu ambamo Yusufu, Mariamu na mtoto Yesu walikuwa wanakaa. Waliingia ndani na walipomwona Yesu walianguka chini na kumsujudia. Walimpa zawadi tatu: dhahabu, uvumba, (ambayo ni utomvu wa mti ambao hutumiwa katika manukato) na manemane (Hii pia inatoka kwenye mti mdogo wa miiba na imekuwa ikitumika katika manukato au dawa). ***(Mathayo 2: 11)***<br>• *Waulize watoto kama zawadi hizi ni kama zile ambazo wangempa mtoto mchanga. Eleza kwamba zawadi hizi zilikuwa za bei ghali sana, na ni aina ambazo zilitolewa tu kwa Mfalme. Jadili - kwa nini unafikiri Mamajusi walichagua kumpa mtoto Yesu zawadi hizi? Eleza kwamba ingawa hatuwezi kutoa zawadi kama wale Mamajusi, bado tunaweza kumwabudu Mungu kwa kumshukuru kwa yote ambayo Amefanya na kujaribu kufanya mambo yanayompendeza.*<br>• Baada ya muda, ulikuwa wakati wa Mamajusi kurudi nyumbani. Herode alikuwa amewaomba warudi na kumwambia mahali walipompata mtoto, lakini Mungu aliwaonya katika ndoto wasirudi kwa Herode, kwa hiyo wakaenda nyumbani kwa njia tofauti. ***(Mathayo 2: 12)*** Jadili – Unafikiri Mamajusi walijisikiaje walipokuwa njiani kuelekea nyumbani? Unafikiri waliwaambia nini watu walipofika nyumbani?<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Mamajusi na Yesu. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, kama inabidi, Mstari Muhimu. ***Mathayo 2: 11.*** |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kukumbushia habari.<br>• Mamajusi waliona nini tena angani?<br>• Walijisikiaje walipoiona nyota?<br>• Nyota iliwaongoza wapi?<br>• Nani alikuwa ndani ya nyumba?<br>• Mamajusi walifanya nini walipomwona Yesu?<br>• Walimpa zawadi ngapi?<br>• Taja mojawapo ya zawadi.<br>• Je, Mamajusi walijuaje kwamba wanatakiwa kurudi nyumbani kwa njia tofauti? |

## B12 Habari ya Nne

**Kukimbilia Misri – Habari hii inahusu Mungu kumtunza Mwanae.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alimlinda Mwanae Yesu.<br>• Tunapaswa kumtii Mungu kama Yesu, Mariamu na Yusufu walivyofanya.<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 2: 15***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mathayo 2: 13-23*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize watoto wakuambie kuhusu ndoto zozote walizoota.<br>Wakumbushe watoto kwamba nyakati za Biblia ndoto zilikuwa na maana za pekee. Waulize wakuambie kuhusu ndoto ambazo wamejifunza kupitia habari hii (ndoto ya Yusufu, ndoto ya Mamajusi).<br>Leo tutajifunza kuhusu ndoto nyingine. |
| **FUNDISHA** | • Baada ya Mamajusi kuondoka, Yusufu aliota ndoto nyingine. Katika ndoto, Mungu alimwambia Yusufu kwamba Herode alikuwa amekasirika sana hivyo angejaribu kumuua Yesu. Mungu alimwambia Yusufu kwamba alitakiwa kumchukua Yesu na Mariamu na kukimbilia Misri ili wawe salama. ***(Mathayo 2: 13)*** *Jadili - Unafikiri Yusufu alijisikiaje alipoota ndoto hii?*<br>• Usiku huohuo Yusufu alifanya yale aliyoambiwa na kuipeleka familia yake Misri. Walikaa huko kwa muda hadi waliposikia kwamba Mfalme Herode amekufa. ***(Mathayo 2: 14-15)*** *Jadili - Unafikiri nini kingetokea ikiwa Yusufu hangefanya kama Mungu alivyomwambia katika ndoto? Ilikuwa muhimu sana kwamba Yusufu afanye kama Mungu alivyomwambia afanye. Waulize watoto kufikiria hii ingeleta matokeo gani. Tafakari juu ya ukweli kwamba hawakuhitaji kuogopa.*<br>• *Mungu aliwaambia wanadamu, wanaoitwa manabii, waandike kuhusu kuzaliwa kwa Yesu, miaka mingi kabla ya Yeye kuzaliwa. Mmoja wa manabii hao alikuwa Hosea. Kitabu chake kiko katika Agano la Kale. Aliandika kuhusu Yesu akiwa Misri.*<br>• *Eleza jinsi Mstari Muhimu unavyozungumza kuhusu Yesu kuwa Misri – Mungu alijua kile ambacho Herode angejaribu kufanya muda mrefu kabla hakijatokea. Katika kila jambo lililotokea, Mungu alikuwa akimlinda Mwanawe.*<br>• *Herode alipokufa malaika mwingine alimwambia Yusufu kuwa ni salama kurudi Israeli. Kwa mara nyingine, Yusufu alitii. Sisitiza kuhusu udhibiti na ulinzi zaidi wa Mungu,*<br>• Yusufu, Mariamu, na Yesu walirudi na kwenda kuishi katika mji unaoitwa Nazareti. ***(Mathayo 2: 19-23)*** *Waambie watoto kwamba Yesu alipokuwa akikua Nazareti, sikuzote Aliwapendeza wazazi Wake, majirani zake na muhimu zaidi Baba yake, ambaye ni Mungu.* ***(Luka 2: 52)*** *Wakumbushe watoto kwamba Mungu anataka tufanye mambo yanayompendeza pia. Jambo bora tunaloweza kufanya ili kumpendeza, ni kumshukuru kwa kumtuma Yesu awe Mwokozi wetu na kwa kumwomba msamaha wa dhambi zetu.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br><br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kukimbilia Misri. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, kama inabidi, Mstari Muhimu. ***Mathayo 2: 15.*** |
| **KUMBUKA** | Waulize watoto maswali yafuatayo kama njia ya kukumbushia habari.<br>• Ni nini kilitokea kwa Yusufu baada ya Mamajusi kuondoka?<br>• Mungu alimwambia Yusufu aende wapi?<br>• Kwa nini ilimbidi kwenda huko?<br>• Yusufu alienda na nani Misri?<br>• Walirudi lini nyumbani?<br>• Walienda kuishi katika mji gani?<br>• Yesu alikuwa na mwenendo gani alipokuwa akikua huko Nazareti?<br>• Tunaweza kufanya nini ili kumpendeza Mungu? |

# Maelekezo ya waalimu wanaposahihisha masomo

**MASOMO YA DARAJA LA KWANZA:**

- Kurasa nne kwenye kijitabu kina sehemu za kupaka rangi, kujaza maneno machache au kufanya kazi rahisi kila wiki.
- Alama 20 zimewekwa kwa kila wiki na alama 80 kwa kila mwezi.
- Watoto wanaotumia masomo ya Daraja la kwanza hawatarajiwi kuwa wanajua kusoma vizuri. Hivyo basi, tunatarajia wazazi/ walezi/ viongozi wa madarasa kuwasaidia.

**MASOMO YA DARAJA LA PILI:**

- Kurasa 4 kila wiki kwenye vijitabu.
- Habari ya Biblia ipo kwenye somo. Watoto/ wanafunzi wanapaswa kupata baadhi ya maneno kwenye somo, kupaka rangi, kukamilisha Mstari Muhimu na kadhalika.
- Alama 20 zimewekwa kwa kila wiki na alama 80 kila mwezi masomo yanapokamilishwa kwa usahihi.

**KUSAHIHISHA MASOMO YA WAKATI NA BIBLIA**

**VITU VYA KUTUSAIDIA TUNAPOSAHIHISHA**

Waalimu wanaombwa kwanza:

- Kuangalia kila somo na kusahihisha ipasavyo.
- Toa alama kama ulivyoelekezwa.
- Kila mara, tumia wino wa rangi tofauti kusahihisha na kuweka ALAMA YA VEMA (✔) kwenye jibu sahihi.
- Weka au andika jibu sahihi panapostahili na rekebisha makosa yoyote ya maandishi (spelling errors), lakini hakuna alama zinazoondolewa kwa ajili ya kosa hili.
- Toa alama nusu kwa kila jibu ambalo sio sahihi kabisa.
- Jumlisha alama za mwezi na uziandike kwenye nafasi uliyopewa kwa ajili hiyo.

Ni muhimu kuwa mkarimu kama uwezavyo ili kuwatia moyo watoto/ wanafunzi wafanye masomo ya Biblia. Kila mwezi, ni muhimu kwa mwalimu kuandika maneno ya kutia moyo kwenye nafasi iliyowekwa kwa kila mtoto anayemfundisha. Unaweza kuandika kuhusu kupaka rangi vizuri, kufanya kazi safi, alama alizopata mtoto, uelewa wa masomo wa mtoto na kadhalika.

Tunajaribu kutoa mawazo tofauti kama iwezekanavyo. Maswali, maoni, maneno ya kutia moyo na kadhalika, yote yanaweza kutumiwa kuleta utofauti. Kama maoni au usemi mmoja unatumika kila mwezi, watoto watauona hauna maana tena.

**DARAJA LA KWANZA**

**Maoni ya jumla**

“Neema – Ninafurahi kuwa umeanza masomo haya na natumai unayafurahia. Nimependa sana ulivyopaka rangi.

“Je, huwa unaenda shule? Niambie kuhusu shule yako. Ninatarajia kusikia kutoka kwako siku za karibuni.”

“Hongera sana Pendo! Umepaka rangi kwa ustadi kweli! Je, ilikuwa vigumu kupaka rangi ndani ya picha tu? Ulikosea kidogo ulipokuwa unapaka rangi kwenye baadhi ya sehemu za somo la mwisho.”

**Maoni ya Kiroho**

“Umefanya vyema sana Faraja! Jairo alikuwa na furaha kubwa Yesu alipomsaidia.”

“Jibu zuri sana! Habari ya kifo cha Yesu inahuzunisha lakini cha kufurahisha ni kwamba, alifufuka tena.”

**DARAJA LA PILI**

**Maoni ya jumla**

“Jibu zuri sana Wema!– “Ninauhakika kuwa, walimu wako wanafurahia sana kazi zako huko shuleni!”

“Debora, naona kuwa tutasherehekea siku yako ya kuzaliwa hivi karibuni. Je, una maandalizi yoyote ya siku hiyo? Je, ni maadalizi gani? Uwe na siku njema!”

“Umejitahidi kweli. Lakini kuna makosa madogo. Usisahau kuhakiki majibu yako kila mara. Mtoto mzuri!”

**Maoni ya Kiroho**

“Napenda ulivyompaka rangi Mtoto Yesu akiwa horini. Je, si inapendeza sana Mungu kumtuma Yesu ulimwenguni kwa ajili yetu?”

“Napenda sana rangi ulizozitumia! Ilimbidi Zakaria kulipa gharama ya kutoamini maneno ya Mungu. Hakukosa kuamini maneno ya Mungu tena.”

“Majibu mwafaka kweli! Mtu aliyekutana na Filipo kule jangwani alienda akiwa na furaha kweli. Alisikia na kuamini Habari Njema za Yesu.”

## Kiambatisho A – Daraja la 0 & la Kwanza Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Inyito | Amashusho y'Inkuru |
|---|---|---|
| B7 | Yusufu | **Kuwasili kwa ndugu zake Yusufu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-joseph-brothers/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-kings-queens/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-vegetation/ |
| | | **Benyamini na habari mbaya** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-joseph-reunion/ |
| | | **Msamaha na habari njema** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-joseph-reunion/ |
| | | **Wakiwa pamoja Misri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/preschool-joseph-reunion/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rp-abraham-land/ |
| B8 | Watu ambao Yesu alikutana nao | **Watu ambao Yesu alikutana nao: mwanamke aliyekuwa anaumwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-024-peter-mother-in-law/ |
| | | **Watu ambao Yesu alikutana nao: mtu mwenye ukoma** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-025-jesus-leper/ |
| | | **Watu ambao Yesu alikutana nao: mtu mwenye kupooza** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-026-jesus-paralytic/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-paralysed-man/ |
| | | **Watu ambao Yesu alikutana nao: Mathayo** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-027-matthew/ |
| B9 | Musa | **Kuzaliwa kwa Musa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/sb-baby-moses/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-baby-moses/ |
| | | **Kosa kubwa la Musa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/sb-baby-moses/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-moses-jochebed/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-baby-moses/ |
| | | **Musa aona kijiti kikiwaka moto** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/sb-burning-bush/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-vegetation/ |
| | | **Musa aleta ujumbe wa Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/sb-burning-bush/ |

## Kiambatisho B – Daraja la 0 & la Kwanza Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Inyito | Amashusho y'Inkuru |
|---|---|---|
| **B10** | **Musa** | **Musa na pigo la kwanza** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-plagues-1/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-men2/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-kings-queens/ |
| | | **Musa na pigo la mwisho** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-plagues-2/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-passover/ |
| | | **Musa na kutoka Misri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-moses-cloud/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-red-sea/ |
| | | **Musa amshukuru Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-red-sea/ |
| **B11** | **Musa** | **Mungu atoa chakula** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-food-water/ |
| | | **Mungu atoa ushindi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-amalekites/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-soldiers-guards/ |
| | | **Mungu atoa amri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-sinai/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-objects/ |
| | | **Mungu atoa wokovu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-serpent/ |
| **B12** | **Habari ya Krismasi** | **Yusufu na malaika** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-mary-angel/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-shepherds-angels/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/birth-jesus-preschool/ |
| | | **Mamajusi na Herode** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-wise-men/ |
| | | **Mamajusi na Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-wise-men/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ls-jesus-born/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-christmas-clipart/ |
| | | **Kukimbilia Misri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/rp-abraham-land/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-009-flight-egypt/ |

## Kiambatisho A – Daraja la Pili Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Inyito | Amashusho y'Inkuru |
|---|---|---|
| **B7** | **Yusufu** | **Kuwasili kwa ndugu zake Yusufu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-brothers-1/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-brothers/ |
| | | **Benyamini na habari mbaya** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-reunion/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-brothers/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-brothers-return/ |
| | | **Msamaha na habari njema** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-reunion/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-brothers-return/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-jacob/ |
| | | **Wakiwa pamoja Misri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/joseph-reunion/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/joseph-jacob/ |
| **B8** | **Watu ambao Yesu alikutana nao** | **Watu ambao Yesu alikutana nao: mwanamke aliyekuwa anaumwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-024-peter-mother-in-law/ |
| | | **Watu ambao Yesu alikutana nao: mtu mwenye ukoma** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-025-jesus-leper/ |
| | | **Watu ambao Yesu alikutana nao: mtu mwenye kupooza** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-026-jesus-paralytic/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-paralysed-man/ |
| | | **Watu ambao Yesu alikutana nao: Mathayo** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-027-matthew/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/photos/lumo-jesus-matthew/ |
| **B9** | **Musa** | **Kuzaliwa kwa Musa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/baby-moses/ |
| | | **Kosa kubwa la Musa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-prince/ |
| | | **Musa aona kijiti kikiwaka moto** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-burning-bush/ |
| | | **Musa aleta ujumbe wa Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-burning-bush/ |

## Kiambatisho B – Daraja la Pili Picha kutoka Free Bible Images (FBI)

| | Inyito | Amashusho y'Inkuru |
|---|---|---|
| **B10** | **Musa** | **Musa na pigo la kwanza** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-pharaoh/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-plagues-1/ |
| | | **Musa na pigo la mwisho** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-plagues-1/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-plagues-2/ |
| | | **Musa na kutoka Misri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-plagues-2/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-red-sea/ |
| | | **Musa na Israeli wamshukuru Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-red-sea/ |
| **B11** | **Musa** | **Mungu awapa Waisraeli chakula** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-food-water/ |
| | | **Mungu atoa ushindi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-amalekites/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-soldiers-guards/ |
| | | **Mungu atoa amri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-sinai/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ten-minute-ot-1/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-objects/ |
| | | **Mungu atoa wokovu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/moses-serpent/ |
| **B12** | **Habari ya Krismasi** | **Yusufu na malaika** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-006-joseph-angel/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-001-word-flesh/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/isc-objects/ |
| | | **Mamajusi na Herode** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-008-wise-men/ |
| | | **Mamajusi na Yesu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-008-wise-men/ |
| | | **Kukimbilia Misri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-009-flight-egypt/ |

© Bible Educational Services 2020

www.besweb.com

Registered Charity UK CIO 1186004

Swahili - v1/2023